# KUCHUNGUZA MATUMIZI YA LUGHA KATIKA RIWAYA ZA KISWAHILI: UCHUNGUZI KIFANI WA RIWAYA ZA *VIPULI VYA FIGO* NA *SIRI ZA MAISHA*

**SIDORA JOSEPH KIMAMBO**

**TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA DIGRII YA UZAMILI (M.A KISWAHILI-FASIHI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**OKTOBA, 2015**

## UTHIBITISHO

Aliyetia saini yake hapa chini, anathibitisha kuwa, amesoma tasnifu hii iitwayo **Kuchunguza Matumizi ya Lugha katika Riwaya ya Kiswahili: Uchunguzi Kifani wa *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*** na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza sehemu ya masharti ya kutunukiwa Digrii ya Uzamili (MA) katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

**DKT. MOHAMED OMARY**

**……………………………………….**

**Msimamizi**

**Tarehe……………………**

## HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote sehemu yoyote ile ya tasinifu hii kwa njia yoyote kama vile, kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

## TAMKO

Mimi, **SIDORA JOSEPH KIMAMBO**, nathibitisha kuwa tasinifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada kama hii au nyingine yoyote.

Sahihi: **--------------------------------------------**

Tarehe ……………………………………………

# TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa Mume wangu Mr. F. Foya

## SHUKURANI

Kazi hii ya Utafiti ni mchango wa matokeo ya safari ndefu baina yangu mimi na watu wengine wakiwemo walimu wangu; rafiki na ndugu siyo rahisi kuwashukuru kwa kina kila mmoja na mchango wake kwangu katika kukamilisha kazi hii lakini kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa uhai na afya njema ya kuniwezesha katika kipindi chote cha masomo yangu.

Pili, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa msimamizi wangu wa tasnifu hii, Daktari, Mohamed Omary kwa kunifuatilia kwa ukaribu sana na kuniongoza vyema kwa kila hatua ya utafiti huu bila kusita wala kuchoka kunishauri na kuniongoza kufanya marekebisho ya kazi hii hatua kwa hatua hadi ilipokamilika. Aidha, msaada wa msimamizi huyu, pamoja na moyo wake mkunjufu hauwezi kulipwa wala kufananishwa na kitu chochote, bali jambo la msingi ni kumwombea maisha marefu na afya njema kwani wapo watu wengi wanaohitaji msada wake. Ninachoweza kusema ni kukushukuru sana Baba, Profesa Sengo, Mwenyezi Mungu akulinde, akupe afya njema na azidi kukutumia ili uwasaidie watu wengine.

Tatu, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa walimu wengine wote wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa kunifundisha vizuri na kuniongoza katika kipindi chote cha masomo yangu akiwemo profesa, E. Mbogo, Dr. P. P. Lipembe, Prof. S. Mdee, Dr. H. Simpassa na Dr. Z. Elisifa.

Nne, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wanangu Emmanuel, Patrick, Doreen na Lilian ambao wamenipa moyo na msaada mkubwa kuwa karibu sana na mimi wakati naiandaa kazi hii. Mungu awape uzima.

Mwisho, nawashukuru wanachuo wenzangu walionipa ushauri na kutoa mchango wao mkubwa katika kuikamilisha kazi hii. Wanachuo hao ni Rehema Adam, Gladys Madoffe na Roxana Mhando. Si rahisi kumtaja kila mmoja kwa kina bali nawashukuru wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine katika kufanikisha kazi yangu.

**Asanteni sana**

**IKISIRI**

Riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha* ni riwaya mpya, kwa maana ya riwaya za karibuni zenye kusheheni matukio ya kusisimua na kutoa mafunzo kwa yeyote aliyewahi ama atakayezisoma aidha kwa kujiburudisha au kujifunza. Ni kazi nzuri na za kuvutia za Profesa Emmanuel Mbogo. Utafiti huu ulifanywa kwa lengo la kuchunguza matumizi ya lugha katika riwaya hizi mbili na kuibua dhamira mbalimbali zilizojitokeza. Utafiti huu ulikuwa na malengo mahususi matatu ambayo ni, kuchambua matumizi ya lugha ya kitamathali katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*, kuchambua matumizi ya lugha yasiyo ya kitamathali katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha* na kuwasilisha dhamira zinazojitokeza katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*. Katika kutimiza malengo haya, tulikusanya data kwa kutumia mbinu za usomaji makini na upitiaji wa nyaraka maktabani na kufanya uchambuzi wa data kwa kutumia mbinu ya mkabala wa kimaelezo na nadharia ya Simiotiki.

Maokeo ya utafiti yanaonyesha kwamba, matumizi ya lugha yaliyojitokeza katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha* ni tamathali za usemi na zisizo tamathali za usemi. Matumizi ya lugha ya kitamathali ni tashibiha, tashihisi, tafsida, sitiari, kejeli na dhihaka. Matumizi ya lugha yasiyokuwa ya kitamathali ni misemo, nahau, takriri, tanakali sauti na taharuki. Pamoja na matumizi haya ya lugha ya kitamathali na yasiyokuwa ya kitamathali pia kuna dhamira mbalimbali zimejitokeza katika riwaya tafitiwa. Dhamira hizo ni biashara haramu, umuhimu wa elimu katika jamii, Dhamira ya malezi katika jamii, hali ngumu ya maisha, siasa na uchumi na nafasi ya mwanamke katika jamii.

# YALIYOMO

UTHIBITISHO ........................................................................................ ii

HAKIMILIKI ........................................................................................ iii

TAMKO ........................................................................................ iv

TABARUKU ........................................................................................ v

SHUKURANI ........................................................................................ vi

IKISIRI……. ........................................................................................ viii

YALIYOMO ........................................................................................ ix

**SURAYA KWANZA ........................................................................................ 1**

**UTANGULIZI ........................................................................................ 1**

1.0 Utangulizi wa Jumla ........................................................................................ 1

1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti ........................................................................................ 1

1.2 Tamko la Tatizo la Utafiti ........................................................................................ 5

1.3 Lengo Kuu la Utafiti ........................................................................................ 5

1.3.1 Malengo Mahususi ya Utafiti ........................................................................................ 5

1.3.2 Maswali ya Utafiti ........................................................................................ 6

1.4 Umuhimu wa Utafiti ........................................................................................ 6

1.5 Mipaka ya Utafiti ........................................................................................ 7

1.6 Mpangilio wa Tasinifu ........................................................................................ 7

1.7 Hitimisho ........................................................................................ 8

**SURA YA PILI ............................................................................................ 10**

**MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA ....... 10**

2.0 Utangulizi ............................................................................................ 10

2.1 Maana ya Riwaya ................................................................................ 10

2.2 Historia na Chimbuko la Riwaya ya Kiswahili ........................................ 13

2.3 Kazi tangulizi Juu ya Riwaya ya Kiswahili ............................................ 15

2.3.1 Kazi Tangulizi za Fani ya Riwaya ya Kiswahili .................................... 15

2.3.2 Kazi Tangulizi za Dhamira katika Riwaya ............................................ 20

2.3.3 Kazi Tangulizi Kuhusu Riwaya za Emmanuel Mbogo ............................ 24

2.4 Mkabala wa Kinadharia ........................................................................ 25

2.4.1 Nadharia ya Simiotiki ......................................................................... 25

2.5 Hitimisho ............................................................................................ 27

**SURA YA TATU ........................................................................................ 28**

**MBINU ZA UTAFITI ................................................................................. 28**

3.0 Utangulizi ............................................................................................ 28

3.1 Umbo la Utafiti ..................................................................................... 28

3.2 Eneo la Utafiti ...................................................................................... 29

3.3 Kundi Lengwa la Utafiti ........................................................................ 29

3.4 Sampuli na Mbinu za Uteuzi wa Sampuli ............................................. 30

3.5 Mbinu ya Uteuzi wa Madhumuni Maalumu ........................................... 30

3.6 Data za Utafiti ...................................................................................... 31

3.6.1 Data za Msingi/Awali .......................................................................... 31

3.6.2 Data za upili ........................................................................................ 31

3.7 Mbinu za Kukusanya Data ........................................................................ 32

3.7.1 Usomaji Makini ........................................................................................ 32

3.7.2 Upitiaji wa Nyaraka ................................................................................... 33

3.8 Uchambuzi wa Data ..................................................................................... 33

3.9 Maadili ya Utafiti ......................................................................................... 33

3.10 Hitimisho ................................................................................................... 34

**SURA YA NNE ..................................................................................................... 35**

**UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI .. 35**

4.0 Utangulizi ................................................................................................... 35

4.1 Wasifu wa Emmanuel Mbogo ...................................................................... 35

4.1.1 Muhtasari wa Riwaya ya *Vipuli vya Figo* .................................................. 36

4.1.2 Muhtasari wa Riwaya ya *Siri za Maisha* .................................................... 37

4.2 Matumizi ya Lugha ya Kitamathali katika Riwaya Teule ........................... 38

4.2.1 Matumizi ya Tashibiha katika Riwaya Teule ............................................. 38

4.2.2 Matumizi ya Tashihisi katika Riwaya Teule .............................................. 40

4.2.3 Matumizi yaTafsida katika Riwaya Teule .................................................. 44

4.2.4 Matumizi ya Sitiari katika Riwaya Teule ................................................... 46

4.2.5 Matumizi yaKejeli au Kinaya katika Riwaya Teule ................................... 48

4.2.6 Matumizi ya Dhihaka katika Riwaya Teule ............................................... 50

4.3 Matumizi ya Lugha Isiyokuwa ya Kitamathali ........................................... 51

4.3.1 Matumizi ya Misemo katika Riwaya Teule ................................................ 51

4.3.2 Matumizi ya Nahau katika Riwaya Teule .................................................. 54

4.3.3 Matumizi ya Takriri katika Riwaya Teule .................................................. 55

4.3.4 Matumizi ya Tanakali Sautikatika Riwaya Teule ........................................ 57

4.3.5 Matumizi ya Lugha yaKitaharuki katika Riwaya Teule ............................. 59

4.4 Dhamira katika riwaya ya *Vipuli vya Figo*na *Siri za Maisha* ...................... 62

4.4.1 Biashara Haramu ......................................................................................... 63

4.4.2 Umuhimu wa Elimu katika Jamii ............................................................... 65

4.4.3 Malezi katika Jamii........................................................................................ 68

4.4.4 Siasa na Uchumi katika Jamii...................................................................... 70

4.4.5 Nafasi ya Mwanamke katika Jamii............................................................. 71

4.5.6 Hali ngumu ya Maisha katika Jamii ........................................................... 75

4.6 Hitimisho ........................................................................................................ 76

**SURA YA TANO ....................................................................................... 78**

**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ......................................... 78**

5.0 Utangulizi ....................................................................................................... 78

5.1 Muhtasari ........................................................................................................ 78

5.1.1 Matumizi ya Lugha ya Kitamathali katika Riwaya Teule ........................... 78

5.1.2 Matumizi ya Lugha yasiyo yaKitamathali katika Riwaya Teule ................ 79

5.1.3 Dhamira katika Riwaya Zilizoteuliwa ......................................................... 79

5.2 Hitimisho ........................................................................................................ 79

5.3 Mapendekezo ................................................................................................... 80

**MAREJELEO ........................................................................................... 82**

# SURAYA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Utangulizi wa Jumla

Wataalamu wengi wa fasihi ya Kiswahili wamefanya tafiti mbalimbali zikiwemo za kuchunguza matumizi ya lugha katika riwaya, tamthilia, na ushairi kwa ujumla, lakini tafiti hizo kwa upande mwingine bado hazijagusa uteuzi wa lugha kwa namna inavyotumika kulingana na makusudio ya mwandishi (Wamitila, 2002).Kwa maana hiyo, utafiti huu umefanywa kama sehemu mojawapo ya kuchangia kujazia pengo la utafiti ili kukuza na kuimarisha utafiti hasa katika riwaya ya Kiswahili. Sura ya kwanza imeelezea vipengele vya kiutangulizi kama vile; usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, lengo kuu na madhumuni mahususi ya utafiti. Aidha maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na mpangilio wa tasnifu pia vimewasilishwa katika sura hii.

## 1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Binadamu katika kuishi kwake anakutana na mambo mbalimbali ambayo hana budi kupambana nayo ili aweze kuyamudu mazingira anamoishi. Mambo ambayo binadamu hukutana nayo katika maisha ni mengi na yanaweza kuelezwa kwa kutumia utanzu wa fasihi hususani riwaya (Msokile, 1992). Kwa kupitia utanzu wa riwaya mtunzi huiumba na kuifinyanga hadithi yake kwa kutumia usanii unaowajenga wahusika wake kwa kutumia kanuni na taratibu za uzuri,upendezaji, uozo na ubaya na kwa hiyo humwathiri binadamu katika kuvuta ama kuchukiza milango yake ya fahamu(Khamis, 2007).

Hata hivyo, Senkoro (1982) anatoa ufafanuzi wa kina wa utanzu huu na kuelezea kuwa, visa na matukio ndio msingi na uti wa mgongo wa riwaya ya Kiswahili na nyingeine zote duniani. Kisa ndiyo sehemu ya asili ambayo imekuwepo toka wakati wa ngano hadi katika riwaya. Vilevile, visa na matukio hayo yanayowahusu wahusika na matendo yao huelezwa kwa mchangamano na mwingiliano mkubwa ambao si rahisi kuupata katika utanzu mwingine wowote wa kazi ya fasihi kama ushahiri na tamthiliya. Aidha, kuwepo kwa utanzu wa riwaya katika kuelezea maisha na matukio anayopambana nayo mwanadamu hakumaanishi kutokuwepo kwa utanzu mwingine wa fashihi ya kiswahili na fasihi kwa ujumla duniani kote. Ndungo (1991) katika maelezo yake anaamini kuwa, fasihi simulizi ni sehemu ya fasihi ambayo ni ya zamani sana ambayo masimulizi yake yalihifadhiwa katika maandishi. Kwa upande wa riwaya, Msokile (1992) anasisitiza kwa kusema kwamba, utanzu wa riwaya ulianza kustawi wakati wa mageuzi ya viwanda na utamaduni huko ulaya. Kwa maana hiyo, utanzu huu ulizuka baadaye sana ukilinganishwa na tanzu nyingine za kifasihi Kama vile, ushairi na nyimbo. Utanzu huu ulizuka wakati maalumu wa historia ya jamii, wakati huo jamii ilikwisha kuwa kubwa yenye makao maalumu na lugha ya jamii hiyo ilikuwa imekwisha pevuka kiasi cha kuweza kueleza dhana, imani na amali mbalimbali za jamii kwa wasanii.

Mlacha na Madumulla (1991) wanaeleza kuwa, historia ya riwaya ya Kiswahili haikupishana sana na hali hiyo ya kutanguliwa na tanzu nyingine za fasihi ingawa kwa hakika umejitokeza mapema zaidi kabla ya tamthiliya ya Kiswahili. Maelezo haya yanaonyesha kuwa, utanzu wa riwaya ulikuwepo tangu zama za kale lakini ukawa umefungamanishwa katika tungo za kishairi simulizi hususani katika tenzi.

Kwa maelezo haya,inaonyesha kwamba,utanzu wa riwaya uliokuwepo ndani ya ushairi uliokuwa bado haujafahamika kwa maana ya uainishaji wake ambao leo hii unafahamika kutokana na kazi kubwa waliyoifanya wataalamu wa fasihi ya Kiswahili.

Uainishaji wa riwaya za mwanzo ni zile zilizoandikwa mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa (19) kutokana na matumizi ya hati za Kilatini na Kiarabu kutumika kuandika na kusoma katika madarasa(Ndungo, 1991). Riwaya zilizoandikwa kipindi hicho zilihusu masimulizi na fikra za ki-magharibi lakini kwa lugha za Kiswahili. Miongoni mwa waandishi wa mwanzo kuandika riwaya ya Kiswahili ni Shaaban Robert. Baadhi ya kazi zake za mwanzo ni riwaya ya *Kusadikika, Adili na nduguze, Maisha Yangu Baada ya Miaka Hamsini, Siku ya Watenzi* Wote na *Siti binti Saad*. Visa na matukio pamoja na uchangamano uliomo ndani ya riwaya, huelezwa kwa kutumia lugha ya kisanii. Mlacha na Madumulla (1991) wanaeleza kuwa, lugha ni kipengele muhimu sana kinachotegemewa na wahusika walivyoundwa, lengo la dhamira pamoja na maudhui yaliyoko katika kazi ya fasihi. Mlacha na Madumulla (1991) wanasema kwamba, umuhimu wa lugha ni katika kuchambua riwaya na kufanya uhakiki kimuundo sio katika utamu, urahisi au ugumu wake. Muundo wa lugha hujumuisha vipengele vingi vya lugha kama vile tamathali za semi, misemo, methali, taswira zilizojitokeza pamoja na dhamira kuu.

Umuhimu wa kuangalia lugha kipekee ndimo yanamojitokeza mawazo ya juu na ya ukito ya mwandishi. Kuangalia lugha katika muundo ukito ni kuangalia maana za ndani za maneno au sentensi ambazo zinaweza kujitokeza pamoja na kuwa maana za kawaida zitakuwa zimepewa uzito wake katika kuiangalia lugha katika muundo wa

jamii (Wamitila, 2008).Baada ya kufahamu maelezo ya wataalamu hawa wa lugha, tukaona ipo haja ya msingi ya kufanya utafiti wa kina wa kuchunguza matumizi ya lugha kama yalivyotumika katika riwaya mbili ambazo ni *Siri za Maisha* na *Vipuli vya Figo*.

Kimsingi, uchunguzi wa kifasihi katika riwaya zilizoandikwa na Emmanuel Mbogo haujafanyiwa utafiti wa kina zaidi ya baadhi ya waandishi kuishia katika kuzitaja tu baadhi ya Riwaya za mwandishi huyu pale wanapoandika vitabu au utafiti kwa lengo la kushadadia hoja na malengo yao. Njogu na Chimerah (1999), Wamitila (2008) na Madumulla (2009) ndio baadhi ya waandishi waliozitaja riwaya hizi katika uchambuzi wao walioufanya kwa malengo tofauti nay a utafiti huu. Tumejaribu kutafuta sababu ya hali hi na kubaini kuwa Emmanuel Mbogo ni mwandishi maarufu zaidi katika tasinia ya tamthiliya kuliko riuwaya na hivyo watafiti na wahakiki kadhaa wakavutiwa katika kuchunguza tamthiliya za Emmanuel Mbogo kuliko riwaya (Massoud, 2013). Sababu nyingine ni kuwa mwandishi huyu aliondoka Tanzania na kwenda Kenya alikofundisha katika Vyuo Vikuu kadhaa na hivyo kusahaulika Tanzania katika ulimwengu wa riwaya.

Ni baada ya kurudi Tanzania katika miaka ya 2000 na kuandika riwaya yake ya Watoto wa Mama Ntiliye ndiposa alipotambulika kuwa ni mwandishi wa riwaya. Riwaya hii ni maarufu na inasomwa kama kitabu cha kiada katika shule za sekondari kidato cha tatu na nne na kama kitabu cha ziada katika kidato cha tano na sita na vyuo vikuu. Kwa kipindi alichokaa Tanzania amefanikiwa kuandika riwaya nyingine za *Vipuli vya Figo* na *Siriza Maisha* lakini hakuna mtafiti hata mmoja mpaka kufikia

sasa ambaye amechunguza matumizi ya lugha katika riwaya hizi mbili. Utafiti huu wetu umeona kwamba hili ni pengo la utafiti na umefanywa ili kuziba.

## 1.2 Tamko la Tatizo la Utafiti

Riwaya ni kazi ya sanaa inayotumia lugha ya kinathari ambapo inaweza kuwa masimulizi ya mtu ya kweli au ya kubuni. Ni kazi ya mtu ama ya mwandishi yenye mwigo wa kiyakinifu ambao umefungamana na wakati, mazingira na mfumo wa jamii (Msokile, 1992).Utafiti na uhakiki wa riwaya ya Kiswahili umefanywa na watafiti kadhaa ambao ni Nkwera(1981) na Madumulla(2009), Senkoro(1982), Senkoro na Kahigi(2006), Mulokozi (1996) na Wamitilla (2002). Kati ya watafiti wote hao hakuna hata mmoja kwa mujibu wa ufahamu wangu aliyeteua kipengele cha lugha na kukitathimini ili kuona namna kilivyotumika katika kazi za kubuni za riwaya za mwandishi Emmanuel Mbogo kama sehemu ya madhumuni ya kazi zao. Utafiti huu umefanywa kwa lengo la kuzibapengo hilo kiutafiti kwa kuchunguza matumizi ya lugha katika kazi za kubuniza *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha.*

## 1.3 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza matumizi ya lugha katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri zaMaisha.*

### 1.3.1 Malengo Mahususi ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na malengo mahususi yafuatayo:

i. Kuchambua matumizi ya lugha ya kitamathali katika riwaya za*Vipuli vyaFigo*na*Siri za Maisha*.

ii. Kufafanua matumizi ya lugha yasiyo ya kitamathali katika riwaya za*Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha.*

iii. Kuwasilisha dhamira kutoka katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri zaMaisha*.

### 1.3.2 Maswali ya Utafiti

i. Ni vipengele gani vya matumizi ya lugha ya kitamathali vilivyotumika katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*?

*ii.* Ni vipengele gani vya lugha isiyo ya kitamathali vilivyofafanuliwa katika riwaya za*Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha?*

*iii.* Ni dhamira zipi zilizowasilishwa katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha?*

## 1.4 Umuhimu wa Utafiti

**Kitaalimu:** Matokeo ya utafiti huu yatakuwa marejeleo muhimu kwa wasomi wa ngazi zote za taaluma ya fasihi ambao ni walimu, wahadhiri na maprofesa katika taalimu ya fasihi. Kwa walimu wa wanafunzi wa sekondari, utafiti huu ni muhimu kwani watautumia katika kuhakikia na kuchambulia vipengele vya lugha katika kazi za fasihi.

**Kinadharia:** utafiti huu utaonesha kwamba upo uhusiano wa moja kwa moja baina ya matumizi ya lugha uwasilishaji wa dhamira mbalimbali katika kazi za riwaya. Hili litabainika pale ambapo katika utafiti huu tumebainisha namna lugha ya kitamathali na isiyo ya kitamathali zilivyotumiwa na mwandishi katika kuwasilisha dhamira mbalimbali. Utafiti huu umetumia nadharia ya Simiotiki katika kuchambua data zake

na hivyo watafiti wengine wa baadaye wataona namna nadharia hii inavyotumika katika kuchambua data na wao wakaitumia kwa namna kama hii au nyingine katika uchambuzi wa data za utafiti wao.

**Kijamii:** utafiti huu utakuwa na umhimu mkubwa katika jamii kutokana na kueleza kwake masuala muhimu katika maendeleo ya jamii. Kwa mfano, katika utafiti huu tumeeleza umuhimu wa elimu katika jamii, malezi katika jamii, athari za biashara haramu na masuala ya siasa na uchumi. Mambo haya ni muhimu katika maendeleo ya jamii na kwa hiyo wanajamii watakaopata fursa ya kuisoma kazi hii watafaidika na maarifa haya na watakapoyatumia watajipatia maendeleo.

## 1.5 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umeshughulikia vipengele vya lugha, jinsi vilivyotumika katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha* tu kati ya riwaya nyingi zilizoandikwa na Emmanuel Mbogo. Matumizi ya lugha yaliyochunguzwa katika utafiti huu ni yale ya kitamathali na yasiyo ya kitamathali tu. Tunafahamu kuwa matumizi ya lugha ni taaluma pana ndio maana tukateua aina hizi mbili za matumizi ya lugha ili kufanikisha malengo mahususi ya utafiti wetu. Uchambuzi uliofanywa katika utafiti huu ni wakifasihi ambapo umeongozwa na nadharia teule ya uhakiki wa kifasihi ambayo ni nadharia ya Simiotiki.

## 1.6 Mpangilio wa Tasinifu

Tasinifu hii ina jumla ya sura tano ambapo katika sura ya kwanza kumeelezewa vipengele vya kiutangulizi katika utafiti. Vipengele hivyo ni pamoja na utangulizi wa jumla, usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, lengo kuu la utafiti,

malengo mahususi ya utafiti na maswali ya utafiti. Vipengele vingine ni umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, mpangilio wa tasinifu na hitimisho. Sura ya pili ni mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Vipengele vilivyowasilishwa katika sura hii ya pili ni pamoja na utangulizi, maana ya riwaya na historian a chimbuko la riwaya. Vipengele vingine ni kazi tangulizi katika fani ya riwaya ya Kiswahili, kazi tangulizi katika dhamira za riwaya ya Kiswahili na kazi tangulizi katika riwaya za Emmanuel Mbogo.

Sura iliyofuatia ni ya tatu ambayo imewasilisha mbinu za utafiti ikiwemo utangulizi, umbo la utafiti, eneo la utafiti, kundi lengwa la utafiti na sampuli na mbinu za uteuzi wa sampuli; mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalumu. Vipengele vingine ni data za utafiti; data za msingi na data za upili na mbinu za kukusanyia data; usomaji makini na upitiaji wa nyaraka. Vipengele vingine ni uchambuzi wa data, maadili ya utafiti na hitimisho. Sura ya nne imewasilisha vipengele vya utangulizi, matumizi ya lugha ya kitamathali yaliyohusisha tashibiha, tashihisi, tafsida, sitiari, kejeli na dhihaka. Matumizi ya lugha yasiyo ya kitamathali yaliyohusisha misemo, nahau, takriri, tanakali sauti na taharuki. Pia katika sura hii ya nne kumewasilishwa dhamira za biashara haramu, umuhimu wa elimu katika jamii, malezi katika jamii, siasa na uchumi, nafasi ya mwanamke na hali ngumu ya maisha katika jamii. Sura ya tano ndiyo ya mwisho ambayo imetoa muhutasari, hitimisho na mapendekezo.

## 1.7 Hitimisho

Katika sura hii tumefafanua vipengele vilivyoonesha haja ya kufanyika kwa utafiti huu. Aidha, tumeonyesha na kubainisha pengo la utafiti na kisha kujenga hoja ya kufanyika kwa utafiti huu. Kwa fahamu zangu, hakuna utafiti wa kina ambao

umefanyika katika ngazi ya uzamili wa kutathimini lugha kama alivyo itumia Emmanuel Mbogo katika kazi zake mbili za kubuni za*Vipuli vya Figo* na*Siri za Maisha.* Kwa sababu hiyo, tukaona kwamba kuna haja ya msingi ya kufanya utafiti huu katika ngazi ya uzamili ili kuziba pengo hili la kiutafiti kwa kuchunguza matumizi ya lugha katika kazi za kubuni za*Vipuli vya Figo*na *Siri za Maisha.*

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.0 Utangulizi

Sura hii imejadili utalii wa maandiko yanayohusu mada iliyofanyiwa utafiti. Katika sehemu hii, tumesoma na kuchambua kazi za watafiti waliotangulia; tukitarajia kupata maarifa na ujuzi utakao tuwezesha kuendelea na utafiti wetu. Katika kusoma kazi hizo, wataalamu mbalimbali wanatoa maelezo gani kuhusu riwaya ya Kiswahili kwa ujumla. Aidha, utafiti huu umetupatia maarifa ya kubaini pengo la utafiti pamoja na nadharia zilizotumika katika kuongoza kuchambua data za utafiti. Hivyo basi, sura hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni maana ya riwaya, historia na chimbuko la riwaya ya Kiswahili. Aidha, katika sura hii tumewasilisha nadharia kadhaa zilizotumika katika kuongoza uchambuzi wa data za utafiti.

## 2.1 Maana ya Riwaya

Maana ya riwaya imefafanuliwa na wataalamu mbalimbali wa lugha na kila mmoja akitoa maelezo yanayotofautiana na mwingine katika vipengele vinavyounda riwaya kwa ujumla. Baadhi ya wataalamu walioelezea dhana ya riwaya akiwemo Senkoro (1982) amefafanua riwaya kwa kusema kwamba, riwaya ni kisa mchanganyiko ambacho huweza kuchambuliwa na kupimwa kwa mapana na marefu kifani na ki-maudhui. Ni hadithi ndefu ya kubuni yenye visa vingi, wahusika zaidi ya mmoja na yenye mazungumzo na maelezo yanayozingatia kwa undani na upana. Riwaya inatoa picha yote ya ujumla ya maisha ya mtu toka nyumbani hadi katika kiwango cha taifa na hata dunia nzima.

Mlacha na Madumulla, (1991) wametoa maelezo ya dhana ya riwaya na kusema: riwaya ni hadithi iliyotungwa ambayo ina urefu wa kutosha, visa vinavyoana na ambayo imezingatia swala la muda. Ukubwa wa riwaya unaweza kuwa kurasa zozote kwani si idadi ya maneno au kurasa tu ambavyo vinatufanya tuiite hadithi fulani kuwa ni riwaya na nyingine kuwa ni hadithi fupi. Wataalamu hawa wa Lugha wametoa maelezo ya kina zaidi pale walipolinganisha riwaya zenye maneno machache kama riwaya ya *Nyota ya Huzuni*(1981) yenye maneno 54,000 na ile ya Bwana Muyombekele na Bibi Bugonoka (1980) yenye maneno 195,000 na kusema kuwa bado zote hizo ni riwaya. Kwa uhakika, maneno haya yanatia changamoto kwa wasanii wanaoibukia na uandishi wa riwaya na hadithi fupi, kwamba riwaya siyo lazima iwe na maneno mengi kama ilivyo riwaya ya Bwana Muyombekele na Bibi Bugonoka (Msokile, 1992).

Pamoja na maelezo ya wataalamu hao, Nkwera (1981) amezingatia vigezo vinavyoijenga riwaya na kusema, riwaya ni hadithi iliyo ndefu kutosha kufanya kitabu kimoja au zaidi. Habari iliyomo ni ya kubuniwa tu, na imejengwa juu ya tukio la kihistoria. Yaweza kuandikwa kwa maelezo ya ujazo (au nathari) au kwa mtindo wa ushairi. Riwaya ni hadithi iendayo mfululizo na kwa kinaganaga. Hueleza maisha ya mtu au kikundi cha watu katika jumla yao au vipengele fulani fulani vya maisha yao. Kila riwaya ina mhusika wake mkuu mmoja au hata wawili. Maelezo haya kwa upande mwingine yametiliwa mkazo na Mlacha (1989) pale alipoonyesha umahiri wa mtunzi wa riwaya kwa jinsi anavyoonyesha usanii katika kazi yake kiasi cha kuifanya jamii iamini kile wasichoamini na kukubaliana na mawazo ya mwandishi.

Kwa upande wake Mlacha (1989) anaeleza kuwa riwaya ni hadithi ambayo imekitwa kwenye dhamira moja kuu. Dhamira hiyo inaweza kuwa imejengwa na dhamira kadhaa pamoja na visa tofauti. Dhamira hizo ndogo kama vile visa, huwa vinahusiana katika kujenga riwaya nzima. Vilevile, riwaya sio maelezo halisi ya maisha ya binadamu bali ni maelezo ya mtunzi kuhusu anavyoyaona maisha ambayo angetaka yawe hata ambavyo angependa yasiwe. Kwa hivyo, riwaya ni mchanganyiko wa ukweli wa maisha na ubunifu wa mwandishi uliojengwa kiasi cha kumfanya msomaji ahusishe hadithi hiyo na maisha halisi ya binadamu. Pia, riwaya huzingatia maisha ya jamii wakati huo. Zaidi ya hayo, mawanda ya riwaya ni mapana zaidi kuliko yale ya tanzu nyingine za kifasihi.

Msokile (1992) anashadidia kwa kusema kwamba, hadithi hutofautiana kutokana na uwezo wa msanii na lengo ama mazingira ambayo hadithi hiyo husimulia au kuandikwa. Katika msingi huo, uwezo wa fanani ama mwandishi ni nyenzo muhimu sana katika ujenzi wa fani na maudhui ya hadithi. Hadithi hizo huzingatia kanuni ama taratibu maalumu za kisanaa. Hali hiyo huifanya hadithi iwe tofauti na kazi nyingine za kisanaa ama zisizo za kisanaa zinazotumia lugha. Hadithi kama kazi ya kisanaa hutumia lugha yenye semi, tamathali za semi, nahau na kadhalika, ili kuwasilisha matendo na mawazo ya wahusika. Wamitila (2000) anasema kwamba, riwaya ni kazi iliyoandikwa kwa mtindo wa kinathari ambayo ina urefu wa kiasi fulani, ni pana, inauchangamano wa kimtindo na kidhamira na inashughulikia masuala kadha katika mtazamano mpana wa wakati.

Wahakiki wa fasihi za ulaya wanatumia kigezo cha idadi ya maneno na kusema kuwa, riwaya lazima iwe na idadi ya maneno yasiyopungua 60,000. Akipingana na

kauli hiyo, Wamitila anasema kwamba, kigezo kama hiki hakifai tunapoziangalia kazi za fasihi ya Kiswahili. Kwanza ni kazi chache sana ambazo zina idadi hiyo ya maneno. Baadhi ya hizo ni *Asali chungu*, na *Kiza katika* Nuru za S.A.Mohamed, *Mwisho wa kosa* ya Z.Burhani, *Vipuli vya Figo* ya E.Mbogo, *Haini* ya Shafi A.Shafi, *Mapenzi yaMukajanga* na *Bwana Muyombekele na Bibi Bugonoka* ya A.Kitereza. Hii inamaanisha kuwa hatuwezi kukitegemea kigezo cha idadi ya maneno kuelezea maana ya riwaya ni riwaya chacehe tu zenye sifa hii. Kwa mfano, kazi mbili za Euphrase Kezilahabi, *Nagona* na *Mzingile* hazina idadi kubwa ya maneno lakini ni riwaya. Ili kuwainisha utanzu wa riwaya tunategemea vigezo kama urefu, uhusika wa kina, uchangamano wa mtindo na uzito wa kidhamira, mwanda wa hadithi, suala la wakati na matumizi mapana ya mandhari (Ndungo, 1991).

## 2.2 Historia na Chimbuko la Riwaya ya Kiswahili

Senkoro (1982) anaeleza chimbuko la riwaya ya Kiswahili na kusema kwamba, ni utanzu wa fasihi uliozuka kutokana na hali mahususi za kijamii. Utanzu huu ulizuka baadaye sana na umefungamana na historia ya mtu. Riwaya za mwanzo ni kama ile ya Kiingereza ya Robinson Crusoe iliyoandikwa na Daniel Dafoe. Riwaya hii ilizuka kutokana na maendeleo na mageuzi ya kiutamaduni na viwanda. Suala la ukoloni na uvumbuzi pia liliumba hali ambazo zilihitajikuelezwa kwamawanda mapana zaidi ya yale ya ngano na hadithi fupi. Hapohapo kuzuka kwa miji na viwanda pamoja na maendeleo ya usomaji yaliyofanya riwaya nyingi ziandikwe. Kwa maana hiyo mawazo na maelezo ya mtaalamu huyu yanatuambia kwamba kwenye uvumbuzi wa viwanda ndio ulioleta chimbuko la riwaya.

Mawazo na maelezo ya Senkoro (tulishamtaja) kwa upande mwingine yanaweza yasikidhi hoja ya chimbuko la riwaya ya Kiswahili kutokana na kuegemea upande mmoja ambao ni mageuzi ya viwanda na utamaduni. Suala la kujiuliza ni je, wakati mageuzi ya viwanda yanafanyika huko Ulaya, Afrika hapakuwa na shughuli yoyote ya kijamii kama masimulizi ya mdomo hata kama hapakuwa na maandishi? Hata hivyo, mazingira ya kuzuka kwa riwaya huko Ulaya yatakuwa yanaihusu jamii ya huko na mazingira yake kwa ujumla, kwa hiyo, mawazo hayo hayawezi kuchukuliwa na kuingizwa kwenye chimbuko la riwaya ya kiswahili.

Mlacha na Madumulla (1991) wametoa maelezo yao na kusema kwamba, historia ya riwaya ulimwenguni haina muda mrefu sana,hasa inapolinganishwa na historia ya tanzu nyingine za fasihi kama vile ushairi, tamthiliya na fasihi simulizi. Maelezo haya yanaonyesha kukubaliana na ya Senkoro (ameshatajwa) kwamba, historia ya chimbuko la riwaya imetokana na uvumbuzi wa viwanda huko Ulaya, baadaye ikifuatwa na riwaya ya Kiswahili. Msokile (tulishamtaja) anaeleza kwamba, chanzo cha riwaya katika fasihi ya Kiswahili ni hadithi na ngano. Bibi au babu alikuwa anakutana na wajukuu na kutambiana hadithi kwa nia ya kushauri, kuonya, kutahadharisha na kuelezana mambo mbalimbali kuhusu jamii. Hadithi hizo zilipokezanwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya masimulizi ya mdomo pasipo kuandikwa.

Senkoro (1976) anaeleza kuwa, historia ya chimbuko la riwaya ya Kiswahiliiilianza wakati James Mbotela alipoandika *Uhuru waWatumwa*(1934). Hii ndiyo iliyokuwa riwaya ya kwanza ya Kiswahili; nayo ilikuwa na mandhari ya huku huku Afrika

Mashariki. Wahusika walikuwa Waswahili na maudhui yake yalihusu Waswahili na mwandishi mwenyewe alikuwa Mswahili.

## 2.3 Kazi tangulizi Juu ya Riwaya ya Kiswahili

Wapo watafiti kadhaa ambao wamechunguza na kuhakiki kazi mbalimbali za riwaya ya Kiswahili katika vipengele vya kimaudhui na kifani. Katika sehemu hii tumefanya mapitio ya kazi tangulizi zinazohusiana na dhamira na fani ya riwaya ya Kiswahili ili kuweza kubainisha pengo la kiutafiti.

### 2.3.1 Kazi Tangulizi za Fani ya Riwaya ya Kiswahili

Fani ni ule ufundi wa kisanaa ambao mwandishi wa kazi ya fasihi huutumia katika kuumba kazi yake na kuipa uwezo wa kuwasilisha dhamira zilizokusudiwa kwa hadhira yake (Wamitila, 2008). Fani ya kazi ya fasihi hutofautiana kutoka mwandishi mmoja na mwingine kulingana na uwezo wake katika ubunifu. Vipengele vya fani katika kazi ya fasihi ni mandhari, wahusika, muundo, mtindo na matumizi ya lugha. Wapo wataalamu kadhaa ambao wamechunguza vipengele hivyo vya fani katika riwaya ya Kiswahili wakiwa na malengo tofautitofauti.

Khatibu (1986) aliainisha tamathali za usemi katika makala yake aliyoiandika katika *Mulika* namba 18, na kueleza kuwa tamathali hizo hutumika katika tanzu mbalimbali za fasihi zikiwemo riwaya, tamthiliya, ushairi, hadithi fupi na fasihi simulizi. Tamathali za usemi alizozitaja ni tashibiha, tashihisi, chuku, sitiari, takriri, simango, kejeli, misemo, taashira, nasihi, tanakali sauti na ritifaa. Uaninishaji huu wa tamathali za usemi ni mzuri na umefungua ufahamu wetu kwa kutuainishia tamathali nyingi za usemi ambazo tumezichukua baadhi yake na kuzitumia katika utafiti wetu.

Hata vivyo, uainishaji huu wa tamathali za usemi umefanywa kwa ujumla sana kiasi kwamba, hata misemo ambayo si tamathali za usemi inatajwa kuwa ni tamathali ya usemi. Misemo ni kipengele cha matumizi ya lugha kinachojitegemea na kinaweza kusimama peke yake katika kuchunguzwa kifasihi. Kipengele cha matumizi ya misemo katika riwaya teule tumekitumia katika uchambuzi wa data za utafiti wetu kama kipengele kisicho cha kitamathali.

Utunzi wa riwaya ya Kiswahili ni makala iliyoandikwa na Kezilahabi (1983) ikieleza mambo mengi yanayotakiwa kuzingatiwa na mtunzi wa riwaya wakati anatunga kazi yake. Moja katika ya mambo ya muhimu yanayotakiwa kuzingatiwa na mwandishi ni ujengaji wa mandhari katika kazi yake. Anaeleza kwamba katika utunzi wa riwaya kuna mandhari ya aina mbili ambayo ni mandhari ya kubuni na mandhari halisi.Kezilahabi anaeleza kuwa matumizi ya mandhari halisi katika kazi ya fasihi ni kazi ngumu sana ikilinganishwa na matumizi ya mandhari ya kubuni. Mandhari halisi inahitaji visa, matukio na wahusika ambao wanafungamana nayo. Kwa mfano, mtunzi anapoteua mandhari ya kijijini ni wahusika, visa na matukio vifungamane ili kufanya maudhui yaeleweke kwa hadhira. Haiwezekani mtunzi anaeleza masuala ya kijijini lakini anatumia mandhari ya mjini na wahusika wenye hulika na tabia za kimjini.

Maelezo haya yanatoa mchango mkubwa katika kufanikisha utafiti wetu kutokana na kule kutaja kipengele cha mandhari na vile kinavyotakiwa kutumika katika kazi za fasihi. Tumefahamishwa kwamba, matumizi ya vipengele vya fani katika kazi za fasihi hutegemeana na kukamilishana. Mandhari ni lazima ifungamane na vipengele vingine vya fani na bila ya shaka matumizi ya lugha ya kitamathali ni lazima

yafungamane na vipengele vingine vya fani. Katika utafiti wetu tumekuwa makini na suala hili na ndipo tukafanikiwa kuchambua vipengele mbalimbali vya tamathali za usemi.

Maelezo ya Kezilahabi hapo juu yanakaribiana sana na ya Mulokozi (1990) anayeeleza kuwa katika utunzi wa riwaya ya Kihistoria mwandishi anatakiwa kuwa makini katika uteuzi wake wa wahusika. Wahusika anaowateua ni lazima wafungamane na kile anachokieleza. Ikiwa mwandishi wa riwaya anazungumza kuhusu Azimio la Arusha basi ni lazima wahusika anaowatumia wafungamane na Azimio la Arusha. Maelezo haya pia ni ya kweli na tunakubaliana nayo na yametusaidia sana kuelewa kwamba, hata tamathali za usemi katika kazi za fasihi hutumiwa kulingana na muktadha uliopo na si vinginevyo. Katika utafiti wetu tumechunguza matumzi ya lugha ya kitamathali katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*.

Matumizi ya sitiari katika riwaya ya *Rosa Mistika* ni uhakiki uliofanywa na Mlacha (1989) na kufanikiwa kuibua sitiari za aina tofautitofauti. Moja kati ya sitiari alizoziiubua ni, "mwezi mkubwa ukimwangalia mlangoni." Katika hali ya kawaida mwezi hauwezi kumtazama mtu lakini hapa imetumiwa kisitiari kumanisha kuwa mhusika Rosa ambaye ni mhusika mkuu katika riwaya hiyo alikuwa akifanya mambo akidhani kuwa ni siri lakini kumbe mambo hayakuwa hivyo? Watu waliomzunguka Rosa walikuwa wanafahamu nyendo zake vizuri kuliko yeye alivyofikiri na kudhani. Maelezo haya yametufanya tuelewe namna sitiari zinavotumiwa na waandishi wa kazi za fasihi na kuwa kazi rahisi kwetu kuchambua sitiari katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*.

Mjema (1990) aliaandika makala iliyochunguza matumizi ya lugha na dhamira katika riwaya ya *Kusadikika*. Katika makala yake hayo alibainisha kwamba, mtunzi wa Kusadikika metumia matumizi ya lugha ya kejeli, mafumbo na kebehi. Pia ameainisha vipengele vya muundo, wahusika na mandhari. Matumizi ya kebehi yanayojitokeza katika Kusadikika ni kule kutumia mandhari ya nchi inayoelea angani lakini mambo yanayofanyika katika nchi hiyo ni yale yanayotokea katika nchi za ulimwengu wa kawaida. Matumizi ya kebehi kwa kawaida humvutia msomaji kuisoma kazi mara tena ili aweze kuelewa kazi hiyo inazungumzia nini hasa. Makala ya Mjema (ameshatajwa) imekuwa na mchango mkubwa wa kufanikisha utafiti wetu kutokana na kututajia baadhi ya vipengela vya matumizi ya lugha na visivyo vya matumizi ya lugha katika riwaya ya *Kusadikika*. Vipengele hivi tumevichukua na kuvifanyia kazi katika utafiti wetu ambapo tumechambua vipengele vya kitamathali za usemi na vingine visivyo vya kitamathali.

Mhochi (2000) alifanya uchunguzi wa matumizi ya mbinu ya usimulizi katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* na kubainisha aina tatu za usimulizi ambazo ni usimulizi maizi, usimulizi wa nafsi ya kwanza na usimulizi wa nafsi ya pili. Anaeleza kuwa katika riwaya hiyo amebaini kuwa mwandishi ametumia usimulizi wa aina zote tatu na kuifanya kazi yake kuwa nzuri na yeye kumvuta msomaji kuisoma tena na tena. Hii inaifanya kazi hii kuonekana kuwa si maneno ya mtu mmoja tu ndiyo yanayojitokeza bali ni maneno ya watu mchanganyiko kwa kutumia nafsi tatu za usimulizi.Katika utafiti wetu tumeweza kuchambua matumizi ya lugha ya kitamathali katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siriza Maisha* kwa kutazama ni nani anayetumia matumizi hayo ya lugha, je ni mwandishi au anatumia wahusika wake.

Kufahamu kauli katika tamathali za usemi zimetolewa na wahusika au mwandishi ni jambo muhimu la kumwezesha msomaji kuelewa vizuri dhamira zilizokusudiwa.

Khamis (2007) alichunguza mitindo mipya katika uandishi wa riwaya ya Kiswahili ya kisasa. Katika kazi yake hiyo anaeleza kuwa kazi za riwaya ya Kiswahili ya kisasa kuna matumizi ya vipengele vya kifani ambavyo vina mwelekea wa kiuhalisia mazingaombwe. Si jambo la ajabu kuona mtunzi akitumia wahusika ambao ni wa ajabuajabu kama majini, mashetani, mazimwi, mtoto anayezaliwa tu na kuanza kuongea na kadhalika. Matumizi ya lugha katika riwaya hizi yale yenye kuonesha mtu kutokuwa na uhakika na maisha yake na wakati mwingine ni lugha ya kukata tamaa. Matumizi ya lugha ya tamathali za usemi yanajitokeza pia katika riwaya za kisasa zikiwa na sifa ile ile ya uhalisia ajabu au uhalisia mazingaombwe. Mawazo ya utafiti wa Khamis (ameshatajwa) yametusaidia katika kufanikisha utafiti wetu ingawa ulikuwa na malengo tofauti nay a utafiti wetu.

Abdallah (2014) alifanya utafiti wa riwaya za Kiswahili za *Kuli* na *Vuta n'kuvute*. Katika utafiti huo alichunguza dhamira za kiutamaduni na zakijamii na kubaini kuwa, riwaya zinatoa mchango mkubwa wa kukuza na kujenga maadili ya jamii. Utafiti alioufanya Omari (tulishamtaja) umetusaidia kubaini kuwa, dhamira haziwezi kuibuliwa bila ya kuwapo kwa lugha ya kitamathali inayomsukuma mwandishi katika kuibua dhamira hizo. Hivyo basi, utafiti wake umetupa ujuzi wa kubaini lugha ya kitamathali inayotumika katika riwaya za Kiswahili. Hata hivyo, lengo la utafiti wetu ni kuchunguza namna Emmanuel Mbogo alivyotumia lugha ya kitamathali katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha* jambo ambalo halijafanyiwa utafiti kutokana na riwaya hizo kuchapishwa miaka ya karibuni.

### 2.3.2 Kazi Tangulizi za Dhamira katika Riwaya

Utafiti tangulizi katika riwaya ya Kiswahili umechunguzwa na wataalamu mbalimbali kwa malengo na nia tofautitofauti. Dhamira ni yale mawazo makuu ya mwandishi ambayo anataka wale wanaosoma kazi yake wayapate (Njogu na Chimerah, 1999). Dhamira katika kazi za fasihi zimegawanyika katika aina mbalimbali ambazo ni dhamira za kijamii, kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi. Kazi tangulizi zifuatazo zimechunguza dhamira hizi kwa kila mtafiti kuwa na lengo lake ili kufanikisha kile alichokusudia.

Sengo (1973) aliandika makala aliyoipa jina la "Dhima ya Fasihi kwa Maendeleo ya Jamii," na kubainisha kuwa fasihi ina jukumu kubwa katika kufunza maadili katika jamii. Kazi ya kufunza maadili katika jamii ilikuwa ni kazi ya fasihi Simulizi kupitia vipera vyake vyote lakini leo kazi hiyo si ya fasihi Simulizi peke yake bali pia ni dhima ya fasihi Andishi na riwaya ikiwa ni miongoni mwao.Akitolea mfano wa riwaya ya *Maisha Yangu na Baada ya Miaka 50* ya Shaaban Robert anaeleza kuwa katika riwaya hii mwandishi amewasilisha vizuri dhamira ya utu wa kibinadamu kuwa ni kitu muhimu katika maendeleo ya jamii. Hakuna jamii yoyote ile duniani ambayo inaweza kupata maendeleo kama haiheshimu misingi ya utu wa kibinadamu. Ikiwa katika jamii watu kunaheshimiwa misingi ya utu jamii hiyo itakuwa na usawa na haki kwa watu wake wote.

Maelezo haya ni muhimu sana katika kufanikisha utafiti wetu kutokana na kutudokezea dhamira zinazopatiana katika riwaya ya Kiswahili ya *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*. Katika utafiti wetu pia tumebainisha dhamira mbalimbali kutoka katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*.

“Shaaban Robert Mwandishi wa Riwaya,” ni mada ya tasinifu ya Uzamili iliyoandikwa na Kezilahabi (1976). Katika tasinifu yak hiyo ameelezea dhamira mbalimbali zinazowasilishwa na katika riwaya za *Kusadikika*, *Kufikiria*, *Wasifu wa Siti Binti Saad* na *Mapenzi Bora*. Mapenzi bora si riwaya ni kitabu cha mashairi lakini kulingana na mambo yanayoelezwa katika kitabu hicho yana uzito mkubwa kimaudhui na ndio maana Kezilahabi aliamua kukitumia kitabu hiki pamoja na riwaya. Dhamira maarufu inayojitokeza katika kazi za riwaya za Shaaban Robert ni dhamira ya ukombozi kutoka katika ukandamizaji unaofanywa na serikali ya kikoloni na hata baadhi ya viongozi wa sasa wa serikali. Serikali ya kikoloni ilichukuwa ardhi ya wananchi yenye rutuba na kuwaachia ardhi isiyofaa kwa kilimo. Pia, serikali ya kikoloni iliwafanyisha wananchi kazi kwa masaa mengi huku wakitoa malipo kidogo kwa wafanyakazi hao wenye asili ya Kiafrika.

Kimsingi, Shaaban Robert katika riwaya zake alitumia mbinu ya kebehi kwa kuelezea madhila yanayofanywa na viongozi katika nchi ya Kusadikika na Kufikirika lakini katika hali halisi viongozi wa leo wanafanya mambo haya haya ambayo yanasawiriwa kujitokeza katika nchi hizo mbili zinazoelea angani. Mawazo haya yametusaidia kupata uelewa kuwa suala la uongozi mbaya katika jamii lina historia ndefu na si la leo. Katika riwaya teule pia mwandishi anatoa mwendelezo wa usawiri wa masuala ya ukombozi na uongozi mbaya katika jamii nasi tumeonesha katika tasinifu yetu ni kwa vipi viongozi wanashindwa kuwatumikia wananchi na badala yake wanajijali wao binafsi.

Mlacha na Madumulla (1991) waliandika kitabu kinachoitwa Riwaya ya Kiswahili na kueleza mambo mengi. Miongoni mwa dhamira waliyoielezea ni suala la ndoa

katika jami ambapo wanakiri kwamba riwaya nyingi za Kiswahili zinaonesha kuwa ndoa ni jambo la muhimu sana kwa jamii za Kiafrika. Baada ya ndoa kinachotegemewa ni kupatikana kwa mtoto na kama mtoto hapatikani lawama hupelekwa kwa mwanamke kuliko mwanamme. Riwaya anayoitolea mfano ni *Bwana Myombekele na Bibi Bugonoka*. Maelezo haya tunakubaliana nayo kwa sababu hata katika jamii ya leo bado suala la ndoa ni muhimu ingawa kuna mabadiliko kidogo ambapo baadhi ya watu hawatilii maanani sana suala la kuoa au kuolewa. Hata hivyo, bado suala hili linapewa kipaumbele sana na watu wengi katika jamii ikilinganishwa na wale wasiolipa kipaumbele. Maelezo haya yametusaidia kuelewa kuwa imani juu ya mila na desturi ni mambo yanayopewa kipaumbele na wanajamii wengi bila kujali kuwa ni wasomi au si wasomi. Katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha* kuna usawiri wa imani juu ya mila na desturi na umuhimu wake kwa jamii.

Naye Shivji (2002) aliandika makala ya hotuba ya uzinduzi wa riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria* iliyoandikwa na Chachage Seith Chachage. Katika uchambuzi wake anaeleza kuwa mwandishi wa riwaya hiyo amesawiri uhalisia wa mambo ulivyo katika tasinia ya uwekezaji ambapo, wawekezaji wanapewa ardhi kubwa yenye rutuba kwa ajili ya uwekezaji na wananchi wanaachwa bila ardhi ya kulima na kufuga mifugo yao. Huu ni unyonyaji wa dhahiri kabisa unaofanywa na viongozi dhidi ya wananchi wao na kuifanya jamii kurudia hali iliyokuwa katika kipindi cha ukoloni. Mawazo ya Shivji yametusaidia sana katika kuielewa riwaya ya *Vipuli vya Figo* na *Siriza Maisha* kwa kuwa nazo zinazungumzia masuala ya unyonyaji wa wananchi na rasilimali zao.

Mohamed (2006) aliandika makala kuhusu mitindo katika riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote* na kubainisha mitindo mbalimbali inayojitokeza katika riwaya hiyo. Matumizi ya mtindo maarufu unaojitokeza katika riwaya hii ule wa matumizi ya uwili katika kila kitu au jambo linalotajwa. Kwa mfano, kila mahali ambapo mwandishi anataja msikiti ni lazima pia ataje kanisa, anapomtaja shehe ni lazima pia amtaje padre na anapotaja wema anataja pia uovu. Matumizi ya mtindo huu yamesaidia kuibua dhamira ya umoja na mshikanamo katika jamii ambapo mwandishi anapendekeza kuwepo na umoja wa dini. Mwandishi anasema kuwa kama kuna umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika na Umoja wa Ulaya kwa nini kusiwe na umoja wa dini ambapo dini za Kiislamu na Kikristo zinaungana na kuwa kitu kimoja. Bila shaka ni jambo linalowezekana na linaweza kuleta mafanikio makubwa katika jamii.

Maelezo haya yanatoa mchango muhimu katika kufanikisha utafiti wetu kutokana na kuelezea umhimu wa umoja na mshikamano katika kuiletea jamii maendeleo endelevu. Hata hivyo, suala la dini za Kiislamu na Ukiristo kuungana na kuwa kitu kimoja ni suala ambalo haliwezekani kutokana na kila dini kuwa na misingi na itikadi ambazo ni tofauti na za dini nyingine.Pamoja na ukweli kwamba dini hizi mbili haziwezi kuungana na kuwa dini moja lakini waumini wa dini hizi mbili wanaweza kushirikiana pamoja katika mambo mbalimbali yanayohusu mustakabali wa maisha yao ya kila siku. Mawazo haya tumeyachukuwa na kuyafanyia kazi katika utafiti wetu uliokuwa umelenga kuchunguza matumizi ya lugha ya kitamathali katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*.

Naye Chuachua (2011) alifanya utafiti wa Shahada ya Uzamili kuhusu "Itikadi katika Riwaya za Shaaban" na kufanikiwa kubainisha itikadi za ukombozi wa kisiasa,

Ujamaa, Ubepari na masuala ya dini. Mwandishi Shaaban Robert amesawiri itikadi hizi akiwa na makusudi ya kujenga dhamira ya utu wa mwanadamu katika jamii. Kwa mfano, itikadi ya Ujamaa anayoisawiri mwandishi ni ile inayolenga kuwafanya wanadamu wote waishi katika maisha ya usawa na haki bila ubaguzi wa aina yoyote. Itikadi ya Ubepari inayosawiriwa na mwandishi ni ile ambayo inasisitiza ubinafsi katika jamii na kwamba kila mtu anatakiwa kuishi maisha yake na familia yake bila kujali masuala ya watu wengine. Itikadi hii inakemewa na mwandishi kuwa haifai hata kidogo kwani inachangia katika kukuza matabaka ya walionacho na wasionacho katika jamii. Mawazo haya ni muhimu sana katika kufanikisha utafiti wetu kwa sababu yanataja itikadi ambazo pia zinapatikana katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha* ambapo kupitia itikadi hizo tumeweza kubainisha dhamira katika riwaya hizo.

### 2.3.3 Kazi Tangulizi Kuhusu Riwaya za Emmanuel Mbogo

Riwaya za mwandishi Emmanuel Mbogo hazijafanyiwa utafiti wa kiasi cha kuridhisha kama ilivyo kwa riwaya za waandishi kama Shaaban Robert, Euphrase Kezilahabi, Said Ahmed Mohamed, Shafi Adam Shafi na Mohamed Suleiman Mohamed. Hata hivyo, wapo watafiti, wahakiki na wananadharia kadhaa ambao wamevitaja vitabu vya riwaya za Emmanuel Mbogo katika kazi na tafiti zao.

Wamitila (2008) ni mwandishi mmojawapo kati ya waandishi wa fasihi ya Kiswahili aliyevitaja vitabu vya riwaya vya Emmanuel Mbogo katika kitabu chake cha *Kanzi ya Fasihi*.Riwaya ya *Watoto wa Mama Ntiliye* ndiyo inayotajwa katika kitabu hicho ikielezewa kuwa ni riwaya ambayo inasawiri hali halisi ya umasikini uliopo katika jamii ya Watanzania. Riwaya hii inasawiri maisha halisi ya mwanamke anayefanya

biashara ndogo ya kuuza chakula katika genge na watoto wake wanavyosakamwa na umaskini hata kushindwa kupata elimu bora katika jamii. Mawazo haya tumeyachukua na kuyafanyia kazi katika utafiti wetu kutokana na ukweli kuwa hali ngumu ya maisha inajitokeza pia katika katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*.

## 2.4 Mkabala wa Kinadharia

Nadharia ni muongozo, utaratibu, kanuni, sheria na miiko ambayo humuongoza mtu katika kulifahamu jambo vile lilivyo au linavyotakiwa liwe (Babbie, 1999). Utafiti unaofanywa kwa kuongozwa na nadharia fulani hupata mashiko ya kitaaluma kwa sababu unaeleza mambo kitaalamu bila kubabaisha na hivyo matokeo ya utafiti huo kuaminiwa na wanataaluma wa fani inayohusika. Katika utafiti huu tumetumia nadharia ya Simiotiki katika kuchambua data za utafiti za malengo mahususi matatu ya utafiti huu lengo likiwa ni kukazia na kuimarisha uchambuzi wa data.

### 2.4.1 Nadharia ya Simiotiki

Simiotiki ni nadharia inayohusika na uchambuzi wa masuala ya lugha inayotokana na na nadharia ya Umuundo iliyoasisiwa na Fednand de Saussure (1966). Nadharia hii kwa ujumla inazungumzia namna lugha inavyotumika kama chombo ya kiishara chenye kuwezesha mawasiliano baina ya watu wawili au zaidi katika jamii. Saussue (ameshatajwa) anaeleza kuwa katika lugha huwa kuna kuwa na vitu viwili ambavyo ni kitaja na kitajwa. Kitaja ni jina linalotaja kitu fulani na kitajwa ndio kile kinachorejelewa na jina hilo. Kwa mfano, neno “kiti,” hili ni jina linalotaja kifaa au kitu cha kukalia ambacho kimeundwa kwa mbao, chuma, godoro au nyenzo nyinginezo. Hivyo, “kiti” ni kitaja na kile kifaa chenyewe halisia kinachorejelewa

ndio kitajwa. Mtaalamu huyu anaendelea kueleza kuwa katika hali ya kawaida hakuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya kitaja na kitajwa bali uhusiano uliopo ni wa kubuni tu.

Ni ukweli ulio wazi kuwa mahusiano yalliyopo baina ya kitaja na kitajwa ni mahusiano dhahania ispikuwa kwa baadhi ya vitu vichache ambavyo majina yao hutokana na mlio wa wao (Blonsky, 1991). Kwa mfano, jina “pikipiki,” hurejelea chombo cha usafiri mithili ya baiskeli lakini ambacho kinatumia moto na ni kutokana na mlio wake wakati imewashwa na kutembea ndio ikapatikana jina hilo. Kitaalamu hali hii hujulikana kama uhusiano wa Kianomatopoea ambao upo katika majina ya vitu vichache tu (Eco, 1984). Kutokana na uhusiano wa majina ya vitu na vitu vyenyewe kutokuwa ni wa moja kwa moja ndipo ile dhana ya kwamba lugha ni sauti za nasibu zilizobuniwa ili kuwezesha mawasiliano katika jamii inapojidhihirisha (Sebeok, 1979).

Wamitila (2002) anaeleza kuwa Simiotiki ni nadharia inayohusika na uchunguzi wa lugha ya picha, ishara, mafumbo na taswira katika kazi ya fasihi. Watunzi wa kazi za fasihi hutumia lugha ambayo si ya kawaida kuelezea matukio ya kawaida katika jamii ili kusawiri hali halisi ya maisha. Kwa mfano, msanii anaweza akasema, “Joyce amenigandaganda mithili ya mdudu kupe hata ninashindwa kufanya kazi zangu kwa ufanisi.” Katika ulimwengu wa kawaida mwanadamu hawezi kumganda mwanadamu mwenzake mithili ya mdudu kupe kwani mdudu huyo ni yule anayekaa katika ngozi ya wanyama na kunyonya damu. Kwa hivyo, kauli hii ni tashibiha iliyotumika kiishara kurejelea mwanamme akilalamika kuwa yeye hamtaki rafiki yake wa kike lakini rafiki huyo haelewi wala hasikii ndio kwanza anafanya kila

linalowezekana kumtaka mwanamme huyo. Nadharia ya Simiotiki ndio inayohusika katika kuchunguza matumizi ya lugha ya ishara na uashiriaji katika kazi za fasihi (Frutiger, 1989).

Matumizi ya lugha ya kiishara na uashiriaji katika kazi za fasihi hujitokeza katika misimbo ya aina tano inayotajwa na Barthes (1994) kuwa ni msimbo wa Kimatukio, Kihemenitiki, Kiishara, Kiseme na Kiutamaduni. Mtunzi wa kazi ya fasihi anaweza kutumia msimbo wowote ule ima msimbo mmoja, miwili au yote mitano katika utunzi wa kazi yake. Katika utafiti huu tumetumia msimbo wa kiishara kwa sababu lugha iliyotumiwa na mwandishi ni ya kiishara zaidi kuliko aina nyingine za misimbo.

## 2.5 Hitimisho

Katika sura hi tumewasilisha mapitio ya kazi tangulizi ambazo zimetoa picha kamili ya utafiti ambao tayari umekwishafanyika katika kuchunguza matumizi ya lugha ya kitamathali na dhamira katika riwaya ya Kiswahili. Mada zilizopitiwa ni Maana ya riwaya, historia fupi ya riwaya ya Kiswahili, kazi tangulizi za fani ya riwaya ya Kiswahili, kazi tangulizi za dhamira katika riwaya ya Kiswahili na kazi tangulizi juu ya riwaya za Emmanuel Mbogo. Kazi tangulizi zote ambazo tumezipitia zinaonesha kuwa hakuna mtafiti hata mmoja ambaye ametafiti matumizi ya lugha ya kitamathali katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*. Katika sura hii pia tumewasilisha nadharia ya Simiotiki ambayo ndiyo iliyotumika katika uchambuzi wa data za utafiti huu.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.0 Utangulizi

Katika sura hii tumewasilisha na kueleza mbinu mbalimbali za utafiti tulizozitumia katika kukusanya data na kuzifanyia uchambuzi. Baadhi ya mbinu zilitumika ni pamoja na umbo la utafiti, eneo la utafiti, aina ya data zilikusanywa na zana za kufanyia utafiti.

## 3.1 Umbo la Utafiti

Umbo la utafiti hutoa picha kamili inayoonyesha namna utafiti ulivyofanyika tangu katika kusanya mpaka kuchambua data za utafiti(Kothari, 2008).Watafiti wengine huita umbo la utafiti kuwa ni usanifu wa utafiti ambao hutoa ramani kamili ya utafiti mzima vile utakavyofanywa katika kukusanya na kuchambua data za utafiti. Utafiti huu umefanywa kwa kuzingatia umbo la uchunguzi kifani ambapo vitabu viwili vya riwaya vimeteuliwa ili kutafitiwa. Uchunguzi kifani ni umbo la utafiti ambapo mtafiti huteua eneo au kitu maalumu ambacho kitashughulikiwa na kuwezesha kupatikana kwa data za utafiti zilizokusudiwa. Katika utafiti huu vitabu vya *Siri za Maisha* na *Vipuli vya Figo* ndio uchunguzi kifani wa utafiti huu ambapo data za msingi zimekusanywa. Uchunguzi kifani ni mbinu nzuri ya kumfanya mtafiti apate data anazozihitaji kwa kuwa humwelekeza mtafiti kukusanya data anazozihitaji (Creswell, 2009). Ukweli huu unamfanya mtafiti kutumia muda mfupi na kufanikiwa kupata data za kutosha tena kwa gharama nafuu kabisa.

### 3.2 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti ni mahali ambapo utafiti unafanyika kulingana na jinsi mtafiti anavyopendekeza ili kupata data za utafiti zitakazomwezesha kujibu maswali ya utafiti (Kothari 2008).Utafiti huu ulikuwa ni utafiti wa maktabani ambao ulihusisha maktaba za jijini Dar-es-Salaam halikadhalika maktaba ya mkoa wa Morogoro. Maktaba za Dar-es-Salaam zilizohusika ni pamoja na maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, maktaba ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, (TATAKI) na maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Katika maktaba hizo, tulipata machapisho mbalimbali tuliyoyahitaji kwa ajli ya kupata data za msingi na za upili za utafiti wetu. Machapisho hayo ni riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*, vitabu mbalimbali vinavyohusiana na mada ya utafiti wetu, majarida, makala mbalimbali pamoja na tasnifu. Hivyo, eneo la utafiti, lililenga upatikanaji wa nyaraka zilizotuwezesha kupata data za utafiti.

### 3.3 Kundi Lengwa la Utafiti

Kwa mujibu wa Robson (2007) sampuli ni jumla ya vitu kama vile wanyama, mimea, milima, matukio mbalimbali au watu kama vile kikundi cha watu na mtu mmojammoja ambavyo mtafiti ameviteua kwa ajili ya kupata data za utafiti wake. Enon (tulishamtaja) anafafanua zaidi kwa kusema kwamba, kundi lengwa ni jumla ya watu wote ambao mtafiti amewalenga na ambao anawategemea kupata taarifa anazozihitaji kwa ajili ya utafiti wake. Kutokana na maelezo haya, kundilengwa la utafiti wetu ni riwaya ya *Vipuli vya Figo* (2008) na *Siri za Maisha* (2010) za Emmanuel Mbogo ambazo zilijadiliwa na kuaminika kuwa mtafiti atapata data za

utafiti na kujibu maswali ya utafiti kulingana na madhumuni mahususi ya utafiti kulingana na madhumuni mahususi ya utafiti huo.

## 3.4 Sampuli na Mbinu za Uteuzi wa Sampuli

Sampuli ni sehemu ya watafitiwa au vitafitiwa vinavyoteuliwa na mtafiti kutoka katika populesheni ya mahali maalumu (Babbie, 1999). Sampuli huteuliwa ili kumwezesha mtafiti kukusanya data anazozihitaji kutoka kwa watafitiwa wachache ambao wanawakilisha jamii pana na kusaidia kupatikana kwa data muafaka za kufanikisha lengo kuu la utafiti. Sampuli ya utafiti huu ni vitabu viwili vya riwaya ambavyo ni *Siri za Maisha* na *Vipuli vya Figo* za mtunzi Emmanuel Mbogo. Ili mtafiti apate sampuli anatakiwa kufanya usampulishaji kwa kuzingatia mbinu mbalimbali za usampulishaji. Kwa maelezo ya Frenkel (1998) anaeleza kuwa, usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kikundi cha watu au vitu kutoka kundilengwa ambalo mtafiti alishaliteua ili litumike kuwakilisha kundikubwa la watu au vitu kwa kuwa siyo rahisi kuteua kundilengwa zima na kulitafiti. Zipo mbinu mbalimbali zinazotumika katika kuteua sampuli kulingana na malengo ya utafiti. Mbinu iliyotumika katika utafiti huu ni uleuzi wa madhumuni maalumu.

## 3.5 Mbinu ya Uteuzi wa Madhumuni Maalumu

Mbinu ya uteuzi wenye madhumuni maalumu ni mbinu ya kuteua sampuli kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa; kwa maana ya vigezo maalumu. Vigezo hivyo ni vile vinavyolenga kujibu maswali ya utafiti. Frenkel (1998) anasema kwamba, mbinu hii ya uteuzi wa madhumuni maalumu ni utenzi ambao mtafiti anaamua mwenyewe kwa hiyari yake kuteua kundi la watu au vitu anavyoamini vinaweza kumpatia data zinazoweza kufanikisha malengo yautafiti wake.

Mbinu ya uteuzui wa sampuli ya uteuzi wa madhumuni maalumu ndiyo iliyotumika katika kuteua riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri zaMaisha* miongoni mwa riwaya za Emmanuel Mbogo. Riwaya hizo ziliteuliwa kutokana na uelewa wa mtafiti kwamba, riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri zaMaisha*, ni riwaya zilizotungwa miaka ya karibuni na kwa uelewa wa mtafiti ni kwamba, hakuna mtafiti aliyezitafiti hasa kwa kuchunguza lugha ya kitamathali ilivyotumika katika riwaya hizo. Kwa maana hiyo, riwaya hizo ziliweza kukidhi mahitaji ya utafiti na kuteuliwa.

### 3.6 Data za Utafiti

Katika utafiti huu tumekusanya data za msingi na upili ili kuwezesha kukamilika kwa malengo mahususi ya utafiti wetu.

#### 3.6.1 Data za Msingi/Awali

Kothari (2008) katika maelezo yake anasema kwamba, data za msingi ni zile zinazokusanywa kwa mara ya kwanza kutoka kwa mtafitiwa. Kwahiyo data halisi ambazo hazijawahi kukusanywa na mtu mwingine yeyote kwa nia na madhumuni ya utafiti. Data za msingi katika utafiti wetu zilikusanywa kutoka katika riwaya za *Vipuli vya* Figo na *Siri za Maisha*. Hii ina maana kuwa utafiti wetu haukuhusisha data za uwandani bali data kutoka vitabuni tu. Tumefanya hivi kwa sababu tuliona kwamba, kwa mujibu wa malengo mahususi ya utafiti wetu yatakamilika kwa kukusanya data kutoka katika riwaya hizo mbili zilizoteuliwa.

#### 3.6.2 Data za upili

Data za upili ni zile ambazo zimekwishakusanywa na watafiti wengine kwa nia ya kukamilisha malengo ya utafiti wao (Robson, 2007). Data za upili zinapatikana

maktabani kupitia vitabu, tasnifu, majarida, tovuti, magazeti, vipeperushi na shajara.Mtafiti huingia maktaba na kuanza kusoma kazi tangulizi kutoka katika vyanzo vilivyotajwa hapo juu kwa lengo la kupata data zinazohusiana na mada ya utafiti wake. Kusoma kazi tangulizi ili kupata data za upili ni kazi endelevu inayoanzia katika kuandika pendekezo la utafiti mpaka kuandika ripoti ya utafiti. Data za upili katika utafiti huu zilisaidia kujaziliza, kuimarisha na kuthibitisha data za msingi ili kufikia lengo la utafiti.

## 3.7 Mbinu za Kukusanya Data

Data za utafiti huu zimekusanywa kwa kutumia mbinu mbili za kukusanya data za utafiti. Data za msingi zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini na data za upili zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya upitiaji wa nyaraka maktabani.

### 3.7.1 Usomaji Makini

Usomaji makini ni mbinu ya kukusanya data za utafiti kwa kusoma kwa kina vitabu au matini zilizoteuliwa ili kupata data za msingi (Yin, 1994). Mbinu hii hutumika kukusanya data za utafiti kwa kuzingatia utaratibu maalumu. Kwanza mtafiti huweka bayana mambo ambayo anakusudia kuyapata kutoka katika matini alizoziteua ili kutimiza malengo yake. Pili anaanza kusoma matini husika na kuirudia mara tena na tena mpaka aielewe vizuri. Tatu anaanza kukusanya data kwa kudondoa katika daftari maalumu aliloliandaa madondoo au nukuu ambazo ndizo data za utafiti zenye kujibu maswali yake ya utafiti. Hivyo, data za msingi za utafiti huu zilikusanywa kwa mtafiti kusoma kwa makini riwaya za *Siri za Maisha* na *Vipuli vya Figo* moja baada ya nyingine na kufanikiwa kukusanya data zilizojibu maswali ya utafiti huu.

### 3.7.2 Upitiaji wa Nyaraka

Upitiaji wa nyaraka ni mbinu ya kukusanya data za upili kutoka katika machapisho mbalimbali yanayopatikana maktabani (Young, 1984). Maktaba ni chanzo sahihi na muhimu ambapo hupatikana na maandiko na machapisho ya aina mbalimbali. Upitiaji wa nyaraka ulifanyika katika maktaba za Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili na maktaba ya mkoa ya Morogoro. Katika maktaba hizi mtafiti alipitia na kusomavitabu pamoja na machapisho mbalimbali kama vile makala, magazeti, tasnifu na tahakiki ambamo aliweza kupata data za upili.

## 3.8 Uchambuzi wa Data

Data zinazokusanywa wakati wa utafiti, hazina budi kufanyiwa uchambuzi kwa lengo la kujibu maswali ya utafiti na kukamilisha lengo lililo kusudiwa(Babbie, 1999). Uchambuzi wa data ni kitendo cha kufafanua data zilizokusanywa ili ziweze kueleweka na kuleta maana iliyokusudiwa (Frenkel, 1995). Kwa maana hiyo data za utafiti huchambuliwa kwa kutumia mbinu stahiki za kiutafiti kutegemeana na aina ya utafiti uliofanyika. Hivyo, mbinu iliyotumika katika kuchambua data za utafiti wetu ni mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo ambapo mtafiti ametoa maelezo ya kina kuhusu matumizi ya lugha katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha* na kuchambua dhamira zilizojitokeza katika riwaya hizo.

## 3.9 Maadili ya Utafiti

Maadili ni dhana pana inayotumika katika mazingira fulani ambapo jamii imejiwekea kwa lengo la kulinda heshima ya amali zake. Maadili ni kama onyo/katazo kuhusu jambo fulani (TUKI, 2004). Kwa maana hiyo maadili ya utafiti

ni onyo linalotolewa kwa mtafiti asifanye mambo fulani kinyume na utafiti unavyotakiwa.Hata hivyo, dhanna hii katika suala zima la utafiti ni muhimu kwa lengo la kuufanya utafiti uaminike, ukubalike kisha utimize malengo yaliyokusudiwa. Kwa hiyo, maadili ya utafiti ni utaratibu wa kuheshimu na kutekeleza zoezi zima la utafiti kwa kutokufanya kinyume na sheria za utafiti. Baadhi ya maadili ya utafiti ni pamoja na kutunza siri au kuhifadhi taarifa zozote zinazotolewa na mtafitiwa/watafitiwa hasa zile zinazomhusu kama vile kutaja jina lake na kumtambulisha katika uchambuzi wa data. Aidha, maadili ya mtafiti yanamkataza mtafiti kupunguza au kuongeza data na kuficha baadhi ya taarifa. Kwa maana hiyo, maadili ya pendekezo la utafiti wetu yalizingatiwa kabla na baada ya kukusanya data na kuhakikisha kuwa taarifa kutoka kwa watafitiwa zinahifadhiwa na kutumika pale zinapohitajika.

## 3.10 Hitimisho

Sura hii imewasilisha masuala ya msingi kuhusiana na mbinu za utafiti tutakazo zitumia katika kukusanya na kuchambua data za pendekezo la utafitiwetu. Hivyo, tumeeleza eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, mbinu za maktabani zilizotumika kupata data kwa kusoma matini mbalimbali zinazohusiana na pendekezo la utafiti wetu. Tumewasilisha pia data mbalimbali za kufanyia utafiti. Vilevile data za msingi zimekusanywa kwa kusoma kwa makini riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*. Vipengele vingine vinavyohusika ni maadili ya utafiti pamoja na hitimisho.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

## 4.0 Utangulizi

Sura hii imebeba mambo mbalimbali ambayo yamegawanyika katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza inahusu utangulizi, na sehemu ya pili ni wasifu wa mwandishi pamoja na muhtasari wa riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*. Na sehemu ya tatu ni uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti kwa kuzingatia malengo mahususi ya utafiti huu. Malengo hayo yalikuwa ni matatu ambayo ni, kuchambua matumizi ya lugha ya kitamathali katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*, kuelezea matumizi ya lugha yasiyo ya kitamathali katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha* na kuchambua dhamira zinazojitokeza katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*. Uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti umefanywa kwa kuzingatia utaratibu huu uliotajwa bila kupindakupinda.

## 4.1 Wasifu wa Emmanuel Mbogo

Profesa EmmanuelMbogo ni mwandishi wa kazi mbalimbali za fasihi,na kazi nyinginezo za kimaadili ya kijamii na kidini.Ni muuminiwadini ya Kikristo,amezaliwa huko mkoani Dodoma.Amefundisha Vyuo Vikuu mbalimbali barani Afrika hususani Afrika mashariki,mfano Chuo kikuu cha Kenyatta huko Kenya na Tanzania amefundisha Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam.Mwandishi huyu ni msomi ambaye daima kalamu yake haiweki chini wala kukauka wino katika kuonya na kuiasa jamii pale inapojisahau au kupotoka kimaadili.Kwa sasa ni miongoni mwa wahadhiri wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na mratibu wa shahada ya Uzamili katika Kiswahili.

Katika kazi zake alizoandika nyingi zina mvuto na zinaleta furaha iliyochanganyika na huzuni, mfano mzuri ni tamthiliya ya *Fumo Liongo* ambapo mtoto wa kambo aliporubuniwa na mfalme amsaliti baba yake na kutoa siri ya nguvu zake.Nyingine ni ile ya *Ngoma yaNg'wanamalundi*,pale nyamiti alipochukuliwa msukule wakati ilikua ni siku moja kabla ya harusi kuanzisha ari,hisia na mori kwa vijana katika harakati za kupambana na wahujumu uchumi,lakini kwa bahati mbaya akafariki ghafla.Huzuni ikaingia kwa wanyonge aliokuwa anawatetea na jamii nzima kwa ujumla.Sio hivyo, tu kiujumla kazi za mtunzi huyu zina mvuto msomaji akianza kusoma kazi moja wapo hataki kuiachia mpaka aone mwisho wake.Msanii huyu ni kipenzi cha watu ni mkweli anawapenda wanafunzi wake kwa kuwaongoza vyema katika kufanya kazi zao za kitaaluma.Baadhi ya kazi zake za tamthiliya ni*Morani* (1997), *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (2008), *FumoLiongo* (2009)*Sundiata* (2011), *Tone la Mwisho* (?) na*GizaLimeingia* (?). Kwa upande wa riwaya ni *Vipuli vya Figo* (2008), *Siri za Maisha* (2010), *Watoto wa Mama N'tilie* (2002) na*Bustani ya Edeni* (?).

### 4.1.1 Muhtasari wa Riwaya ya *Vipuli vya Figo*

Riwaya ya *Vipuli vya Figo* ni hadithi inayoelezea hali ya maisha ya mtu anapokuwa madarakani na hatma yake baada ya kuondoka katika madaraka hayo aidha kwa kuondolewa na serikali kwa mujibu wa sheria, kwa maana ya kustaafu kazi au kuondolewa madarakani kwa njia ya kufukuzwa kazi baada ya kukiuka miiko ya uongozi. *Vipuli vya Figo* ni riwaya ya kiuhalisia. Farihisi katika riwaya hii inasadifu maisha ya jamii pamoja na mambo yote yanayoizunguka jamii hiyo, ili kujiweka kwenye nafasi ya kulinda hesima kwa kuendeleza kufanya mambo maovu hata kama hayakubaliki, siyo tu kwa jamii hiyo, bali hata kwa jami nyingine duniani kote.

Hadithi hii imegawanyika katika sura ishirini na mbili zenye visa na matukio ya hapa na pale yanayosadifu maisha ya kiongozi mwenye wadhifu mkubwa serikalini anayetegemewa kuwa kioo cha jamii lakini badala yake amekuwa mtu wa kutisha, muuaji na mkiukaji wa haki za binadamu.

### 4.1.2 Muhtasari wa Riwaya ya *Siri za Maisha*

*Siri za Maisha* ni miongoni mwa riwaya za Prof. Emmanuel Mbogo. Riwaya hii ina visa na matukio yaliyomkumba mhusika wake mkuu Pama baba wa watoto wawili; aliyetoweshwa kimiujiza na kiumbe aliyejulikana kwa jina la Melkizedeki. Kiumbe huyo hakuwa binadamu bali ni roho iliyojulikana kwa jina hilo. Kutoweka kwa Pama kulileta simanzi, sio kwa mkewe tu, bali hata kwa rafiki zake na mkewe pia.

Kiumbe aliyemtowesha Pama alikuwa na mpango mzuri wa kumsaidia Pama ki-maisha, lakini Pama hakugundua mapema. Mpango wa kumsaidia Pama ulikuwa ni kumfundisha Siri za Maisha baada ya Melkizedeki kugundua kuwa Pama alikuwa na uwezo mkubwa wa kubuni kazi za kujiajiri badala ya kuajiriwa na kulipwa ujira mdogo.Mafunzo aliyoyapata Pama, yalimwezesha kugundua kuwa, kila binadamu ana kipaji akiwemo na yeye mwenyewe: kwamba binadamu hatutakiwi kukata tamaa. Vilevile, alijifunza kuwa maneno yanayo tamkwa na mtu, yana nguvu kubwa ya kuweza kujenga au kubomoa. Maneno hayohayo, ndiyo yanayotumiwa na wazazi au walezi katika kumdhoofisha au kumstawisha mtoto. Maelezo yaliyoko kwenye riwaya hii, yalimjengea Pama ujuzi wa kuweza kuanzisha kiwanda chake kidogo cha kutengeneza vifaa na vyombo vya umeme; ambayo ni kazi aliyoajiriwa kwa Sunche Kapeto. Riwaya hii kwa ufupi inatoa mafunzo kwa mtu aliyekata tama baada ya kupambana na changamoto za maisha zikiwemo mishahara midogo. Kwamba,

binadamu asikate tamaa bali kila mmoja ajiamini kuwa ana uwezo wa kuweza kufanya jambo la kumletea faida.

### 4.2 Matumizi ya Lugha ya Kitamathali katika Riwaya Teule

Lengo mahususi la kwanza la utafiti huu lililenga kuchambua matumizi ya lugha ya kitamathali katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*. Tamathali za usemi ni kauli fupifupi ambazo hutumiwa kisanaa na watunzi wa kazi za fasihi kulinganisha na kufananisha vitu viwili au zaidi vyenye sifa na tabia tofauti kana kwamba ni vitu vinavyofafanana kabisa (Wamitila, 2008). Tamathali za usemi ni nyingi lakini katika utafiti huu tumewasilisha na kuchambua zifuatazo:

#### 4.2.1 Matumizi ya Tashibiha katika Riwaya Teule

Khatibu (1986) anatoa maelezo kuhusu tashibiha na kusema kwamba ni usemi unaolinganisha vitu viwili halisi vinavyoonekana, ambavyo vinaleta mshabaha. Katika tashbiha maneno kama mithili ya, sawasawa na, mfano wa na kana kwamba hutumiwa kufananisha vitu viwili. Emmanuel Mbogo anaendelea kutumia tashbiha ili kuibua dhamira alizokusudia ziifikie hadhira yake kwa kusema

> Alifadhaika, akahamaki, “Pama!’’ Brenda alikimbia akajikuta chumbani kwa watoto. Hakuna Pama. “Pama!” aliita. Kimya. **Macho yake kama jozi ya Kurunzi**, yalimulika huko na kule. (2010:20).

Katika dondoo hili mwandishi amefananisha mwanga uliotoka kwenye macho ya Brenda na ule unaotolewa na kurunzi.Kwa lugha ya kawaida, kurunzi haina jozi ya mwanga, mwanga wake una chanzo kimoja tu; nacho ni betri.Mwandishi ametumia zile betri mbili zinazowekwa kwenye kurunzi na kuelezea kama kila betri inatoa mwanga wake kwenye kurunzi hiyohiyo mojaili kuonyesha ukali wa mwanga

huo.Haya ni matumizi ya mbinu za kisanii za kuweza kuchota dhana fulani kwenye mazingira ya kila siku na kuitumia dhana hiyo kisanii ili kudhihirisha alichokusudia mwandishi.Kwa maana hiyo,mwanga uliotoka kwenye macho ya Brenda ulikuwa mkubwa kiasi cha kuuelezea kwamba hamaki ya Brenda baada ya kumkosa Pama kitandani na kumtafuta katika nyumba yake ilikuwa kubwa sana. Tashibiha hii imejengwa kwa kutumia msimbo wa kiishara ambapo kunatolewa ishara ya mwanga wa kurunzi na kufananishwa na namna Brenda alivyotumbua macho yake baada ya kumtafuta Pama na kummkosa katika kitanda chao chumbani (Blonsky, 1991).

Mwandishi Emmanuel Mbogo anaendelea kutumia tashibiha za usemi katika riwaya ya *Vipuli vya Figo* kama ifuatavyo:

> Alianza **kibao pole pole kama gari moshi** linaloanza kuondoka … Samahani. Lakini siwezi kuacha mpira abadani. **Maneno haya yalikuwa kama shoka iliyopigwa** kwa nguvu katika uso wa nafsi na hadhi ya babu mzazi mzee mwenye nyumba Dkt. Matoga … kimya tena kilipita pale sebuleni Dkt. Matoga akiwa kasimama fikra zikimwenda mbio, **hasira zikitokota ndani kifuani kama volcano** inayotafuta ufa ili itokeze duniani (2008:88).

Dondoo hili linaonesha kuwa Dkt. Matoga alikuwa ni mtu mkali sana kwa watoto na wajukuu wake. Kutokana na ukali huo alimpiga kibao kikali mwanawe mmoja kutokana na mtoto huyo kukataa kumsikiliza baba yake alipomkataza kwenda kucheza mpira. Kibao hicho kinafananishwa na “mlio wa gari moshi linapoanza kuondoka.” Pamoja na kibao hicho mtoto huyo alimjabu baba yake kuwa kamwe hawezi kuacha kucheza mpira. “Majibu hayo yalikuwa ni kama shoka iliyopigwa kwa nguvu katika uso wa nafsi na hadhi ya babu.” Hii ina maana kuwa maneno haya yalimuudhi sana Dkt. Matoga. Majibu ya kijana huyo yalimfanya Dkt. Matoga kupandwa na hasira “kifuani kama volcano iliyotafuta ufa ili itokeze duniani.” Hii

ina maana kuwa, hasira hizo zilikuwa kali sana. Hapa mwandishi ametumia lugha ya ishara akielezea namna mtu anavyopata hasira kubwa kutokana na maudhi aliyofanyiwa mithili yake huwa ni kama volcano inapochemka ndani ya ardhi na kutafuta mahali pa kutokea nje (Eco, 1984). Volcano inapochemka ndani ya ardhi ni lazima itoke nje na hutoka kwa kasi ya ajabu ambayo wakati mwingine husababisha madhara kwa wanadamu, wanyama, mazingira na maisha ya jamii kwa jumla. Hii inaashiria kuwa mtu mwenye hasira anaweza kufanya jambo lolote lile bila kujali na kusababisha madhara kwa kwake mwenyewe na kwa watu wengine pia.

### 4.2.2 Matumizi ya Tashihisi katika Riwaya Teule

Tashihisi ni tamathali ya usemi ambayo hutumiwa na watunzi wengi wa kazi za fasihi kama vile riwaya, tamthiliya, ushairi, hadithi fupi na fasihi simulizi kwa nia mbalimbali mojawapo ikiwa ni kujenga dhamira zinazohusu jamii ambayo mwandishi amekusudia kuiandikia. Msokile (1993) anaielezea tashihisi kuwa ni tamathali ya usemi ambapo vitu hupewa sifa zote au baadhi ya sifa za kutenda kama binadamu na kuonekana kama binadamu. Anaendelea kuielezea tamathali hiyo na kusema kuwa, baadhi ya wataalamu huielezea katika mazingira matatu; kwamba:

- Ni sitiari ambayo huonyesha kitu kisicho mtu kuwa na tabia za mtu.
- Kuichukua sehemu ya umbile la binadamu na kukipa kitu sifa za binadamu huyo.
- Ni sitiari ambayo huwakilisha kitu kisicho hai na kukipa wazo la kiumbe hai.

Maelezo yaliyotolewa na mtaalamu huyu yanasadifu kile alichokichora Emmanuel Mbogo kwenye riwaya ya *Vipuli vyaFigo*, kwamba hapana shaka mwandishi ni

mahiri wa kutumia lugha kisanii ili kujenga dhamira mbalimbali kwa hadhira yake na kuteka hisia za wasomaji wa riwaya hii kiasi cha kujiuliza maswali ambayo majibu yake ni kutamani kuendelea kuisoma kazi hiyo hadi mwisho. Haya yamethibitishwa pale mwandishi aliposema:

> Juu kabisa ya lango hili kuliachwa uwazi wa kama futi mbili zilizokuwa zimetandikwa nondo imara za chuma. Kufuli kubwa zenye uzito wa takribani robo kilo zilizofungwa nchi moja juu, moja chini na moja katikati ya lango la chuma. Kuzunguka gereza hilo ukuta mwingine mrefu wenye seng'enge kama futi kumi na mbili wote ukiwa umejengwa kwa mawe, **ulikuwa ngome madhubuti iliyosimama kwa kiburi kutimiza wajibu wa kuwalinda wafungwa**. Upande kunako tua jua karibu na nyumba walizoishi askari jela, gereza lile lilikata kona likafanya umbo kama namba saba (2008:116).

Katika dondoo hili, mwandishi ametumia tashihisi kuonyesha namna ambavyo gereza lilitakiwa kuwa ili kuwadhibiti wafungwa wasitoroke. Makosa waliyofanya baadhi ya wahusika katika riwaya hii ambao baadhi yao ni Shipe na Mwamvita yaliwafanya wahifadhiwe gerezani. Neno **kiburi** limetumika kitashihisi kuonyesha kitu kisicho mtu kuwa na tabia za mtu. Huo ukuta wa gereza uliojengwa kwa mawe, kisha ukazungushiwa seng'enge, na tena urefu wake ni futi kumi na mbili, maneno yote haya yanaonyesha uimara wa hilo gereza kwamba wafungwa hawawezi kubomoa na kutoroka. Siyo rahisi ukuta kuwa na kiburi, kwani ni binadamu peke yake ndiyo mwenye uwezo wa kuwa na hisia za kiburi, lakini kama ukuta nao umeonekana kuwa na uwezo wa hisia za kiburi, basi ni wazo kwamba, msomaji atakayesoma riwaya hii atataka kujua hawa watu waliowekwa kwenye gereza madhubuti namana hii ni watu wa namna gani, au mwandishi alitaka kuibua dhamira gani hadi atumie tashihisi? Kwa hali hii, msomaji hana budi kutafakari kwa kina ili

aweze kupata dhamira zilizofichwa na mwandishi katika tashhisi hizo (Sebeok, 1979).

Emmanuel Mbogo anaendelea kutumia tashihisi kwa lengo la kusukuma mbele dhamira zilizojitokeza na kuyaweka wazi matukio yaliyoko katika riwaya hii kwa kumpatia msomaji/wasomaji ujumbe uliokusudiwa. Maelezo haya yanathibitishwa na mwandishi kupitia wahusika wake pale aliposema:

> Ingefaa uende kuongea na mzee ili tujue tutafanya nini kabla hatujaadhirika na pata shika za polisi. Mama yao alinyamaza kitambo, akauhisi **uchungu ukiung'ata moyo wake**, joto lilimpanda na kifua kikajaa upepo. Ma Angela aliyasikia **maneno ya bintiye kama miiba ya mchongoma yakitonesha hasira zake dhidi ya mumewe** (2008:11-12).

Kwa kawaida, mtu anapofukuzwa kazi anakumbwa na mambo mbalimbali kama vile kuyumba kiuchumi pamoja na kushuka kwa heshima aliyokuwa anapewa na jamii kabla ya kufukuzwa kazi. Dkt. Matoga baada ya kufukuzwa kazi aliyumba kiuchumi (uk.24) na pia heshima aliyokuwa anapewa ilitoweka na akaonekana kama mtu wa kawaida bila kujali wadhifa aliokuwa nao siku za nyuma. Wakati akiwa kazini, alikuwa na nafasi nzuri serikalini lakini aliendekeza starehe ndiyo maana hakuwa na nyumba yake binafsi ambayo ingeweza kumsitiri kwa wakati huo. Kufukuzwa kazi kwa Dkt. Matoga kulimfanya Ma Angela (mkewe) apatwe na uchungu ambao mwandishi asingeweza kuuelezea kwa undani bila kutumia tashihisi zilizokolezwa wino katika dondoo hapo juu.

Kimsingi, tashihisi hizi zimetumika kwa lengo maalumu la kumfanya msomaji ajiulize maswali kwamba kufukuzwa kazi kwa Dkt. Matoga ndiko kulikomfanya Ma Angela apatwe na uchungu kiasi hicho au kuna mambo mengine yaliyofichika. Je,

mwandishi anataka kuwasilisha nini kwa msomaji. Msomaji anapojiuliza maswali haya, atapata shauku ya kufuatilia kwa makini maelezo ya mwandishi ili apate dhamira zilizokusudiwa kuwakilishwa (Akhmanova, 1992). Kwa maelezo haya tumeona kwamba, mwandishi ametumia lugha ya kisanaa ili aweze kufikisha ujumbe wake kwa jamii iliyokusudiwa. Hii inaonekana pale anaposema, "uchungu ukiung'ata moyo wake," Katika tashihisi hii mwandishi ametumia lugha ya ishara kuonesha uchungu uliompata mke wa Dkt. Matoga dhidi ya mumewe.

Matumizi ya tashhisi katika riwaya ya *Siri za Maisha* yamebeba ujumbe mzito ambao mwandishi kwa kutumia usanii wake anatueleza kwamba:

> **Upepo mwanana wa usiku ule ulipuliza, nayo majani ya maua yaliyumba taratibu**; chamvua ya waridi ikapeperushwa hewani yakamkumbusha Pama manukato ya mkewe Brenda aliyopenda kuyarashia. Oh! Maskini Brenda atakapotanabahi sipo, atahamaniki si haba; Aliwaza na kutupa macho juu alijiuliza mfululizo wa maswali yaliyokuwa hayana majibu saa hizo. **Mbingu ilikuwa bubu** bali ilijitambia utandu na mtandao mkubwa wa anga samawati iliyotonewa na maelfu ya nyota zilizopwitapwita kwa utukufu (2010:15-16).

Katika dondoo hili, tunamwona mwandishi alivyobobea kwenye usanii wa lugha hususani tashihisi,kwamba ametumia tashihisi kwa mfululizo kwenye aya moja katika kuichora mandhari waliyokuwemo ili kuthibitisha yale aliyokusudia (tazama maneno yaliyokolezwa wino).Kama alivyosema Sengo (2009) kwamba,lugha ya sawasawa ikishamkaa mtu, hasiti kuzimudu beti za kila bahari za arudhi ya Kiswahili asilia,Insha za kabila zote, Barua za kuliza na kupoza,za posa na oseo pamoja na tungo aina za kila utanzu na vijitanzu.Maneno ya mtaalamu huyu,yana mantiki na yamesaidia katika kujenga hoja na kuimarisha mawazo yetu.Ni kweli kwamba,wasomaji wa riwaya hii,wanaposoma kwamba vitu visivyo na uhai kama

vile upepo,majani ya maua mbingu,anga na nyota,vyote hivyo vimeweza kufanya vitendo vinavyofanywa na binadamu;vitendo vya kuyumba,kupuliza,kuwa bubu na kupwitapwita,hakika wasomaji hao watajiuliza maswali yatakayowafanya watafakari kwa kina ili waweze kupata kile alichokusudia mwandishi (Barwise na Perry, 1983).

### 4.2.3 Matumizi yaTafsida katika Riwaya Teule

Lugha wakati mwingine hutumia maneno maalumu ili kuonyesha heshima au kupunguza ukali wa lugha. Maneno haya maalumu, yanayotumika kwenye lugha, kwa lugha nyingine wataalamu wa lugha wameyaita adabu katika lugha (TUMI, 1992). Katika matumizi ya lugha, Senkoro (1982) anasema kwamba, tafsida ni tamathali inayojitokeza kwa utumizi wa neno, msemo au nahau ambayo hupunguza ukali au matusi badala ya kutumia neno, msemo au nahau kali kama ya matusi. Akitolea mifano ya maneno ya kitafsida, Senkoro (tulishamtaja) anaongeza kwa kusema kwamba, msemaji wa maneno kama**kukojoa** au **kunya** anatakiwa aseme kwenda **haja** au kujisaidia. Hali kadhalika na neno kufa msemaji aseme **kuaga dunia**. Wakati mwingine, maneno ya kitafsida yanatakiwa yatumike kwa uangalifu vinginevyo inaweza kuonekana kuwa msemaji ana dharau (Msokile, 1993).

Emmanuel Mbogo ni msanii aliyebobea kwenye sanaa ya lugha na kutilia maanani kile kinachoitwa **adabu** katika **lugha** anapoandaa kazi zake za kisanii kama alivyozichora tafsida kwenye *Vipuli vya Figo* na kutueleza kuwa:

> Dkt. Matoga, badala ya kuingia alirudi nyuma na kumung’unya maneno yasiyoeleweka, **akachepuka na kwenda haja ndogo**. Dereva mzee Choma, hata pale aliposimama alisikia **maji ya Waziri wa Afya yaliyomwagika na kutoa harufu ya chumvichumvi** (2008:01).

Kwa hakika, dondoo hili linaonyeha hali halisi ya tabia ya huyu mheshimiwa, kwamba, wadhifa aliokuwa nao haulandani kabisa na tabia yake. Jamii aliyokuwa anaiongoza akiwemo dereva wake asingeweza kujifunza kutoka kwake kwani kiongozi anatakiwa awe mfano wa kuigwa ili aweze kuwaongoza vizuri watu wake. Maneno yaliyokolezwa wino yanaoneshakiongozi akijisaidia mahali ambapo si rasmi na hivyo kuchafua mazingira.Huu ni mfano tu wa viongozi ambao hawafuati sheria, kanuni na taratibu mbalimbali katika kuendesha shughuli zao za kila siku mojawapo ikiwa ni viongozi kujihusisha katika vitendo vya rushwa (Abdallah, 2014).

Mwandishi ameendelea kutumia tafsida pale alipomchora mhusika wake akisema, “alijua lini amkemee mjamzito aliyejilegeza na kulia ovyo wakati wa uchungu wa kujifungua.”Tafsida hii inaonyesha kwamba, mwandishi yuko makini katika matumizi ya lugha hasa anapokuwa katika mazingira ya kuibua dhamira alizokusudia kuifikia jamii husika. Tafsida hii imejengwa kutokana na matumizi ya lugha ya ishara ambapo kujifungua kunaashiria kitendo cha mwanamke kuzaa mtoto. Katika mazingira ya kawaida anayezaa ni mnyama kama ng’ombe na mbuzi na mwanadamu anajifungua. Hivi ndivyo namna watunzi wa kazi za fasihi wanavyotumia lugha kiishara kwa lengo la kujipambanua kutokana na wanyama (Frutiger, 1989).

Akiendelea na matumizi ya tafsida katika kazi zake, mwandishi ametumia tafsida kupitia mhusika wake pale aliposema:

> Brenda alihisi ubaridi ukimtambaa mgongoni badala ya joto Alilozoea. Alitupa mkono huko na huko lakini hakumpata aliyetaka kumpapasa. Alijua kaenda uani kujisaidia, akasubiri. Dakika tano. Vipi? Aliita,” Pama?’’ Kimya; ila sasa mwadhini alisikika toka mbali, sauti yake ilipasua anga la usiku wa alfajiri(2010:19).

Katika dondoo hili, mwandishi ametumia tafsida ili kuondokana na kero ambayo inaweza kumpata msomaji au msikilizaji wa kazi hii ya fasihi. Khatibu (1986) anatoa maelezo ya matumizi ya tafsida katika riwaya ya *Rosa Mistika* (1971)kwamba, katika riwaya hiyo Euphrase Kezilahabi amechora mazingira ya tafsida ambayo yanaficha matusi bila kutamka waziwazi ili kuheshimu miiko ya kimila na desturi ya jamii ya Watanzania.

### 4.2.4 Matumizi ya Sitiari katika Riwaya Teule

Kwa kawaida, wasanii wa kazi za fasihi hawachoki kutumia tamathali za usemi, mbali na kuzipamba kazi zao, wanakuwa na lengo maalumu katika kusaidia kusukuma mbele dhamira zilizojitokeza kwenye kazi zao. Sitiari kama zilivyo tamathali zingine za usemi, hulinganisha vitu vya aina mbili au zaidi vyenye sifa tofauti kama vile ilivyo katika tash-biha. Lakini tofauti na tash-biha, sitiari haitumii maneno ya viungo kama vile: kana, mfano wa, mithili ya, kana kwamba, na kadhalika (Msokile, 1993). Katika kufafanua sitiari, Khatibu (1986) anasema, sitiari ni tamathali ya usemi ambayo hulinganisha vitu vya aina mbili au zaidi vyenye sifa tofauti kama vile ilivyo katika tashibiha. Naye Msokile (1992) anatoa maelezo kuhusu sitiari na kusema kwamba, ni tamathali ya usemi ambayo kwa kawaida inahusianisha matendo, kitu au tabia ya vitu vyenye maumbile tofauti.

Ulinganisho huu unazingatia misingi au sifa inayopatikana katika vitu vyote viwili, lakini sifa hizo haziwi wazi kati ya kitu na kitu. Khatibu (ameshatajwa) anatoa maelezo kuhusu sitiari na kusema kwamba,ni aina nyingine ya tamathali ya semi.Sitiari hutokea kitu kinapopewa jina la kitu kingine. Uhamishaji huu huwa kutoka kwenye aina moja ya kitu au vitu kwa mujibu wa kufanana kwa vitu hivyo.

Maelezo yaliyotolewa na wataalamu hawa ni ya msingi na kwamba, Emmanuel Mbogo ni miongoni mwa waandishi wa kazi za fasihi aliyobobea katika matumizi ya Sitiari ili kujenga dhamira mbalimbali kwa hadhira yake. Katika kutumia tamathali hii anasema:

> Alihofu kuwa mwanaye alipotea nafasi yake nzuri ya masomo na kuwa mtu maarufu maishani kama wazazi wengi Dkt. Matoga alishikilia msemo wa: **Elimu niufunguo wa Maisha**. Lakini kibao alishikilia msemo wa: Elimu ni ufunguo mmoja tu kati ya funguo nyingi zilizoweza kumfungulia mtu milango ya riziki na heri maishani (2008:25).

Katika dondoo hili, mwandishi hakutaka kutumia lugha ya kulinganisha au kufananisha suala la elimu na kitu kingine au jambo lingine, bali aliichora hii sitiari moja kwa moja katika kumaanisha kile alichokiona katika elimu, kwamba ni ufunguo wa maisha. Kwa lugha ya kawaida, ufunguo ni kifaa kinachotumika kufungulia au kufungia kufuli au kitasa cha mlango au kabati (TUKI, 2004:425). Kwa hiyo, kama elimu ni ufunguo wa maisha, mwandishi anataka kuiambia nini hadhira yake? Mwandishi kwa makusudi kabisa ametumia sitiari hii kwa lengo la kuwateka wasomaji wake ili kuibua dhamira zilizojitokeza katika kazi zake (Mrikaria, 2010). Kutokana na matumizi ya sitiari “elimu ni ufunguo wa maisha,” mwandishi anaitaka jamii kuelewa kuwa elimu ni kitu muhimu sana kwa maendeleo ya mtu mmojammoja na taifa kwa jumla.

Mwandishi amekua mstari wa mbele kaika kuichora tamathali ya sitiari ili kusukuma mbele dhamira zilizokusudiwa ziifikie hadhira yake.Katika kuthibitisha kauli hii, amemtuma mhusika wake pale aliposema:

> Muhifadhi maiti aliitwa Nixon. **Nixon alikuwa na kichaka cha ndevu** usoni, macho mekundu kwasababu ya bangi na meno yaliyokoza weusi wa giza. Alikuwa amevaa magwanda ya khaki(2010:52).

Katika dondoo hili,mwandishi amemaanisha alichokiandika;kwamba,Nixon alikuwa na kichaka cha ndevu na siyo vinginevyo.Mwandishi hakutaka kufananisha ndevu za Nixon na kichaka, bali alimaanisha ni kichaka kweli kwa jinsi zilivyomjaa usoni.Hii ni mbinu ya usanii wa hali ya juu katika kunasa hisia za wasomaji waendelee kuisoma kazi yote kwa lengo la kupata dhamira zilizokusudiwa.

Mawazo yanayojitokeza katika mtazamo wa mwana falsafa Sengo (2009) ni kuwa, lugha ya kiswahili imesheheni utajiri mkubwa wa tamathali za usemi ambapo mwandishi yeyote wa kazi za fasihi kwa kutumia usanii wake hawezi kukwama katika kazi zake. Kwa hiyo, tamathali hizo za usemi ni pamoja na sitiari ya Elimu ni ufunguo wa Maisha ambayo mwandishi kwa kutumia usanii wake ameichora kwenye kazi yake kwa lengo la kuibua dhamira alizokusudia ziifikie hadhira aliyokusudia.

### 4.2.5 Matumizi yaKejeli au Kinaya katika Riwaya Teule

Utamu wa lugha haupo tu katika maudhui yaani kile kinachoelezwa bali pia ladha ya lugha huzidi kwa ustadi wa kuyaeleza maudhui yenyewe (Njogu na Chimerah, 1999). Ni katika melezo haya ndiko tunakoweza kubaini kile anachokizungumzia mtaalamu huyu wa lugha; kwamba, waandishi wa kazi za fasihi wanao ufundi wa kuzichora dhamira zilizoko katika kazi zao kwa kutumia lugha ya kisanii hususani kejeli. Wataalamu wa lugha wametoa ufafanuzi juu ya kejeli ikiwa ni miongoni mwa tamathali za usemi, zinazotumiwa na waandishi wa kazi za fasihi katika kuibua dhamira zinazojitokeza katika kazi zao. Senkoro (1982) anafafanua na kusema kuwa,

kejeli ni tamathali ambayo maneno yake huwa kinyume kabisa maana yanayotakiwa kutoa. Kejeli huweza kuchanganya tamathali zingine kama vile za ubeuzi uliofichika, kinyume, tabaini, na msisitizo bayani. Halikadhalika, Msokile (1993) naye anasema, kejeli ni tamathali inayotumia maneno ambayo kwa kawaida huwa kinyume kabisa na maana inayotakiwa kutoa maneno hayo. Akifafanua aina za kejeli, Msokile (tulishamtaja) anasema kwamba, kejeli iko katika makundi mbalimbali ambayo ni: kinaya rahisi, kinaya inayoelezea ajali na kinaya drama.

Kwa maelezo haya, tunaweza kuyaona matumizi ya kejeli jinsi mwandishi Emmanuel Mbogo alivyoitumia katika kusukuma mbele dhamira alizokusudia wakati anamchora mhusika wake akisema:

> Siku hizi ajabu ya Mungu, hata tabia mkuu wa magereza kabadili kila Jumapili kava suti, Biblia na kitabu cha tenzi za rohoni mkononi mara anapoegesha gari kuelekea Cathedral. Mwenyewe Dkt. Matoga Injinia wa uchimbaji mifereji hii ambayo sasa imefurika fedha, akaunti yake ya hapa nyumbani imevimba karibu kupasuka, achilia mbali ile ya Uswizi (2008:192).

Hapa katika dondoo hili, tunaona mwandishi alivyompamba mhusika wake Dkt. Matoga ambaye tayari alishafukuzwa kazi kwa tuhuma za ubadirifu wa fedha za ummalakini mwandishi amemchora kuonyesha jinsi alivyo na fedha nyingi zisizokwisha. Kwa kawaida mfereji hupitisha maji wakati wote, sasa Dkt. Matoga kuitwa, “Injinia wa uchimbaji mifereji ya fedha,” wakati ukweli ni kwamba, fedha aliyokuwa anaipata haikuwa ya halali bali ni kwa njia ya biashara haramu aliyokuwa akiifanya. Dkt. Matoga hakujali utu wa mtu, bali alitanguliza hela mbele kuliko jambo lingine lolote ndiyo maana mwandishi akamchora kama Injinia wa uchimbaji

mifereji ya fedha.Mwandishi anaendelea kutumia kejeli katika kusukuma mbele dhamira alizo kusudia pale alipomchora mhusika wake kwa kusema:

> Mzee alirudi jana?" Aliuliza Alice. "Kama kawaida yake, hakutokea jana" alijibu Chacha na kuongeza kwa kejeli,"naona alikuwa na mkutano mrefu, maana wao ni watu wakubwa ati bwana (2008:4).

Dondoo hili linaonyesha kwamba, mwandishi anao uwezo mkubwa wa matumizi ya kejeli kwani katika kumchora mhusika wake Dkt. Matoga hakueleza huo ukubwa wake kama ni wa umri au waki nadhifa, lakini hata hivyo mtu mkubwa anapokuwa na mkutano kwani unamzuiya asirudi nyumbani? Nadhani ukubwa huo ndio ambao ungemsukuma arudi nyumbani hasa kwa kulinda heshima yake kwa watu wengine. Lakini mwandishi alitaka kuonyesha ni jinsi gani Dkt. Matoga alivyoweka starehe mbele na kusahau wajibu wake kama baba wa familia. Hata hivyo, ufahamu huu wa kuweza kuyatambua mawazo ya mwandishi, yanatokana na ndharia ya Simiotiki ambayo tunaitumia katika utafiti wetu.

### 4.2.6 Matumizi ya Dhihaka katika Riwaya Teule

Senkoro (1982) anafafanua tamathali hii na kusema kwamba, ni aina ya kejeli. Ni tamathali ambayo ina ubeuzi mkali, jahili unaopenya kweli. Hii pia hutumia kutoa maneno ambayo kijuujuu yanahusika vizuri sana masikioni wakati ambapo huwa yamekusudiwa yatoe maana iliyo kinyume chayo kabisa. Maelezo yaliyotolewa na Senkoro (tulishamtaja) kuhusiana na tamathali ya thihaka tunakubaliana nayo kwa asilimia miamoja na kwamba, Emmanuel Mbogo ni miongoni mwa watunzi wa kazi za fasihi ambaye anatumia tamathali za thihaka katika kujenga tamathali mbalimbali zinazojitokeza kwenye kazi zake kama alivyozitumia katika *Siri za Maisha* na kusema:

> Wajua tena nongwa ya Mama Hidaya. Basi najaribu kumweleza juu ya kutoweka kwa baba Sandra lakini wapi. Ameniambia, “Oh! Katoweka! Katoweka nini? Basi huyo mumeo kachukuliwana wenzake wanaojua kuwalea wanaume! (2010:42).

Katika dondoo hili, mwandishi ametumia dhihaka ili kuteka hisia za wasomaji. Aidha, ameonyesha ni jinsi gani tamathali hii inavyotumika kutoa maneno ambayo ni kinyume na ukweli. Kwani katika maelezo ya mwandishi hakuna kipengele kinachoeleza kuwa Mama Sandra alishindwa kumlea mumewake. Msomaji yeyote atakayeisoma tamathali hii kwenye kazi za Emmanuel Mbogo, itakuwa vigumu kwake kukubaliana na yaliyomo kwenye kazi zake kwani yana kinzana na kumfanya msomaji ajiulize maswali kadha wa kadha; kwamba kwanini mwandishi ameamua kutumia maneno yaliyomhusu mhusika wake Mama Sandra ambaye kwa ukweli aliishi vizuri na mumewe. Huu ni usanii wa hali ya juu alionao mwandishi katika kuibua dhamira mbalimbali kwa kutumia lugha ya kitamathali.

## 4.3 Matumizi ya Lugha Isiyokuwa ya Kitamathali

Lengo mahususi la pili la utafiti huu lilikuwa linahusu kuelezea matumizi ya lugha yasiyo ya kitamathali katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*. Lengo hili limefanikiwa kutimizwa ambapo vipengele vya

### 4.3.1 Matumizi ya Misemo katika Riwaya Teule

Watunzi wa kazi ya fasihi, aghalabu hutumia misemo ya aina mbalimbali ambayo kwa dhamira mbalimbali huweza kufikishwa kwa hadhira ilikusudiwa. Senkoro (1982) anasema kwamba, mara kwa mara misemo na nahau katika kazi za fasihi hushabihiana sana nay ale ya methali. Misemo hutumiwa wakati mwingine

kutambulisha mazingira maalumu au kuijulisha hadhira wakati unaohusika katika kazi ya fasihi inayoshughulikiwa. Akiendelea kufafanua dhanna ya misemo, Senkoro (tulishamtaja) anasema kwamba, misemo huzuka ama kuibuka na kutoweka kufuatana na hali mbalimbali za kimazingira.

Kwa hiyo, matumizi ya misemo katika kazi za fasihi hutegemea uhai wa misemo hiyo kwa jinsi inavyotumika katika mazingira maalumu na kuleta maana maalumu. Kwa maana hiyo, misemo katika kazi za riwaya ni mbinu muhimu ya kisanaa ambayo mwandishi anaitumia katika kunasa hisia za wasomaji na kuleta vionjo vya kijamii kwani misemo hiyo haishuki kutoka mbinguni bali inatokana na jamii ambayo mwandishi ameiandikia. Wasomaji wa riwaya wanapokutana na misemo wanayoifahamu inakuwa rahisi kwao kuelewa dhamira zilizolengwa na mwandishi ziifikie hadhira katika riwaya hizo.

Misemo katika riwaya ya *Vipuli vya Figo*, imeipamba riwaya nzima kuanzia sura ya kwanza hadi ya mwisho na kuifanya riwaya hii ieleweke kwa urahisi na kuwavutia wasomaji wake. Mwandishi ametumia misemo katika kazi yake kwa lengo la kusaidia kuwasilisha dhamira alizokusudia pale aliposema:

> Naye alibaki kumshukuru Mungui kuwa alikuwa amekaribia kumwondoa katika ulitima na kumwingiza katika maisha yenye uhakika. Wateja wake wengi isipokuwa wachache, walirudi kwake, nyuso zimejaa furaha, vifua vyao sasa vimesimama wima na bakhishishi ya fedha zaidi au vitenge na kanga. **Lakini kama wasemavyo ng'ombe wa maskini hazai, maskini akiokota huambiwa mwizi**. Saa sita usiku hivi, askari kanzu wawili walipiga hodi nyumbani kwakena alipogoma kuufungua mlango wakauvunja mlango wa kuingia, bastola mkononi (2008:117).

Katika dondoo hili msemo uliotumika kwamba, ng'ombe wa maskini hazai, unavuta hisia za msomaji au wasomaji na kumtambulisha mhusika kuwa, siyo rahisi kwa mtu wa kipato cha chini kuibuka ghafla na kuwa tajiri bila kuwa na nyenzo za kumsaidia mtu huyo katika kuupata utajiri huo, vinginevyo utajiri wa aina hiyo hauwezi kudumu (Mwaifuge, 2006). Hapa tunamwona mhusika Shipe akiwauzia akina mama supu ya mbwa kwa imani kuwa supu hiyo itayafanya matiti yaliyonyonywa yakaanguka yaweze kusimama tena kama vile hayajanyonywa. Kwa kuwa hii ni biashara haramu inayokiuka hala za wanyama na kuwadhalilisha wanawake, ni wazi kwamba, haikumfaidisha mhusika bali mwisho wake ilimwangamiza yeye mwenyewe. Halikadhalika, kupitia dondoo hili, tumefahamishwa kwamba, binadamu ni mtu mwenye tamaa na wa kupenda kupata faida kwa kila jambo analolifanya, kwa hiyo busara ikatumika kabla ya kufanya jambo na zaidi ya hayo ni muhimu mtu kujiwekea mipango mizuri ya maisha kabla ya kutenda jambo (Cherry, 1966).

Mwandishi Emmanuel Mbogo ametumia misemo katika riwaya ya *Siri za Maisha* kwa lengo la kuwasilisha dhamira zake ili ziifikie hadhira aliyokusudia, anasema:

> Melkizedeki najua siwezi kudai kuwa nimekufahamu hasa, lakini haya yaliyomo ndani ya mkoba huu naenda kuyatia katika vitendo. **Mbawa zimemuota Tai, hakuna kitakachonizuia kuruka na kutua kileleni**. Niruhusu nitoe hotuba yangu katika hii mahafali yangu kabla chombo chetu hakijafika (2010:75).

Mwandishi ametumia lugha ya picha na ishara akimaanisha kuwa mtu yeyote yule katika jamii akipata nyenzo za kuzalisha mali anaweza kuondokana na umasikini (Waugh, 1984). Kinachowafanya wanajamii kuendelea kuwa masikini ni kukosa nyezo na vitendea kazi vya kuzalishia mali kutokana na fursa mbalimbali zilizopo katika mazingira yao.

### 4.3.2 Matumizi ya Nahau katika Riwaya Teule

Emmanuel Mbogo ni msanii mahiri wa matumizi ya nahau, anaendelea kuipamba kazi yake na kuwavuta wasomaji waweze kupata vionjo kutokana na nahau zilizo sheheni katika kazi yake. Nahau ni msemo uliojengwa kwa kutumia maneno ya kawaida lakini ambao huwa umesitiri maana tofauti na ile iliyobebwa na maneno hayo katika matumizi ya kawaida. Senkoro (1982) akiendelea kufafanua dhanna ya nahau, Senkoro, (tulishamtaja) anaongezea kwa kusema kwamba, kimatumizi, nahau ni sawa na misemo ila yenyewe ni misemo ambayo huwa imeshika miziz zaidi katika jamii, na hadhara yake ni pana zaidi nahau hutumiwa kupamba kazi za fasihi na pia katika kuwaainisha wahusika na lugha zao.

Nahau pia hutumiwa na wasanii kutajirisha maelezo yao. Kutokana na maelezo ya mtaalamu huyu tunaona kuwa, yote aliyoyazungumza kuhusu nahau yamejitokeza kwenye riwaya ya *Vipuli vya Figo* kama mwandishi alivyosema:

> Watoto wa aina yake walionekana kila siku wakichakurachakura katika majalala miozo ya chakula, maradhi na shibe za aina yake. Mazingira na maisha haya yalinizomea. Dkt. Matoga kila siku aliporejea hapa Mabatini, yakamfunza kuwa:**Mpanda ngazi hushuka**. Lakini naye, kama watu wawili waliokuwa wakijibizana na kulumbana kichwani mwake alijibu falsafa hiyo kwa mapitio ya methali hiyo hiyo, na kwa kejeli ‘Mshuka ngazi hupanda ngazi hadi juu(2008:85).

Katika maelezo ya awali tumeambiwa kuwa, misemo huzuka katika kipindi maalumu kuleta maana maalumu. Ni kipindi hiki ambacho Dkt. Matoga amefukuzwa kazi na kuondolewa kwenye nafasi aliyokuwa nayo, nafasi ya uongozi na kurudi kuwa mtu wa kawaida. Katika dondoo hili, tunatambulishwa kwamba katika maisha kuna mabadiliko; na kwamba mtu anapokuwa kwenye nafasi fulani hasa katika hali ya kupata mafanikio, hana budi kuitimiza na kuithamini nafasi hiyo kwa kutenda yale

yanayokubalika katika jamii, vinginevyo anaweza kujikuta amepoteza nafasi yake na kukosa yale yote aliyokuwa anayafaidi. Dkt. Matoga alipokuwa Waziri, hakuthamini nafasi yake bali aliendeleza starehe akashindwa hata kujijengea kibanda chake ambacho kingeweza kumsitiri alipofukuzwa kazi. Kwa maana hiyo, alijikuta ameondolewa kwenye nafasi ya juu ya uongozi na kurudi chini kuwa mtu wa kawaida.

Aidha, kupitia dondoo hili tumefahamishwa kwamba, kila binadamu ana nafasi yake anayoitegemea katika kuishi ili kumwezesha kupata kile anachokihitaji. Mkulima anayo nafasi yake ya kuongeza bidii katika kazi yake ili aweze kuzalisha zaidi apate faida na mahitaji mengine. Kwa hiyo, mtu anapochezea nafasi yake na kushindwa kuisimamaia vizuri, asitegemee nafasi hiyo ikishatoweka itarudi tena (Sengo, 2009). Kwa hiyo, Dkt. Maoga aliposema "Mshuka ngazi hupanda ngazi hadi juu" (uk.85) alikuwa anajifariji tu na kujutia nafasi yake aliyoichezea lakini hakuna jambo kama hilo. Mwandishi ametumia nahau hii ya, "mpanda ngazi hushuka," kiishara kuonesha kuwa maisha ni kitu chenye kubadilika badilika na hayadumu katika hali moja. Ngazi hapa imetumiwa kurejea jambo tofauti kabisa na dhana ya ngazi iliyozoeleka (Nazarova, 1984).

### 4.3.3 Matumizi ya Takriri katika Riwaya Teule

Waandishi wengi wa kazi za fasihi hutumia mbinu ya takriri katika kazi zao kwa ajili ya kuwasilisha dhamira zilizolengwa ziwafikie hadhira aliyokusudia. Msokile (1993) anaeleza kuwa, takriri ni marudiorudio ya neno, sauti, herufi, au wazo na kadhalika katika kazi ya sanaa ya kifasihi. Marudiorudio ya aina hiyo hufanywa kwa lengo la kuleta athari fulani kwenye ubongo wa msomaji au masikio ya msikilizaji na

kumfanya atilie maanani kile kinacho sisitizwa. Maelezo ya mtaalamu huyu kuhusu takriri yanaumuhimu mkubwa katika kazi za fasihi hasa tukimchukua Emmanuel Mbogo ni miongoni mwa wasanii wanaotumia mbinu ya takriri katika kujenga dhamira mbalimbali kwa hadhira yake. Katika *Vipuli vya Figo* anasema:

> Shughuli ya kushusha mizigo polepole na kwa uangalifu, Dkt. Matoga akiogopa kuvivunja ama kuviharibu vifaa vile vya thamani. Hivyo saa zote alikuwa akitahadharisha, polepole! Polepole! Angalia! Polepole! Nimesema … hadi mizigo yote ikawa imeingia salama (2008:57).

Katika dondoo hili, mwandishi ametumia takriri neno kuonyesha msisitizo na umakini katika kushusha vile vyombo vya thamani. Neno **polepole** limerudiwa mara kadhaa na kumfahamisha mhusika kuwa hivyo vyombo ni vya thamani kubwa nap engine haviwezi kupatikana kwenye mazingira ya jamii ya *Vipuli vya Figo*, hivyo ni muhimu kuwa makini wakati wa kuvishusha. Aidha, takriri iliyotumika, ina mjulisha mhusika kuwa, mbali na kuwa vyombo hivyo ni vya kuvunjika kwa urahisi, vinaweza pia kumwumiza yule anayevishusha, pengine vyombo vingine vina ncha kali au makali yanayoweza kumkata mtu. Kwa maana hiyo, msomaji anapokutana na matumizi ya takriri katika kazi ya fasihi inakuwa rahisi kwa msomaji huyo kile anachokusudia mwandishi, kwa maana ya kuelewa dhamira zilizokusudiwa (Omari, 2009). Vilevile, matumizi ya mbinu ya takriri yamejitokeza pia katika riwaya ya *Siri za Maisha* kwenye sura mbalimbali ili kutia msisitizo wa kile mwandishi alichokusudia kwa kusema:

> Kwa muda wote hawa wawili walikaa kimya lakini hatimaye Pama aliuliza kwa sauti ya wasiwasi, “Wewe nani na unanipeleka wapi?” “Tulia! Tulia! Unanijua bilashaka. Tangu juzi nimekuwa nakwambia mimi ni Melkizedeki (2010:13).

Mbinu ya matumizi kwenye kazi yoyote ya fasihi ni muhimu katika kujenga dhamira kulingana na mazingira ambamo takriri hiyo imetumika. Takriri inatia msisitizo kwa mhusika katika kumruhusu au kumkataza kufanya jambo fulani.Katika dondoo hili, mwandishi ameichora ameichora takriri katika mazingira ya kumtuliza Pama, kwamba kwa muda ule wakiwa katika chombo cha usafiri, hakuruhusiwa kufanya jambo lolote mpaka chombo kitakapotua.Aidha takriri imeendelea kutumika katika riwaya hii pale mwandishi aliposema:

> Pama alishusha pumzi akamwomba aingie Sebuleni Alikataa. “Hapa inatosha” Niingie! Niingie! ya kazi gani? We nipe pesa yangu Niondoke (2010:03).

Katika dondoo hili, mwandishi ametumia takriri neno “niingie,” kuweka msisitizo kwa Pama kumlipa mama Hedaya deni Lake. Msokile (1992) katika maelezo yake anasema kwamba, mtindo huu wa msisitizo una lengo la kufanya jambo limwingie msomaji vyema. Anaendelea kusisitiza kwamba, takriri inatumiwa kupambanua dhamira zilizoko katika hadithi.Wakati huo huo pia takriri inapamba hadithi kisanaa na kusaidia kuweka kumbukumbu ya baadhi ya mambo muhimu; kwa nia ya kutaka kukazia jambo fulani.

### 4.3.4 Matumizi ya Tanakali Sautikatika Riwaya Teule

Matumizi ya tanakali sauti, huonekana kwenye kazi za wasanii wengi wa fasihi kwa lengo la kusukuma mbele dhamira zilizokusudiwa ziwafikie jamii husika. Katika kazi za fasihi, tanakali sauti hutokana na sauti zinazofanana ziundwazo na maneno au nomino (Senkoro, 1982). Tanakali sauti au Onomatopia ni matumizi ya neno ambalo likitamkwa huelekea kutoa maana. Tanakali sauti ni neno ambalo kimsingi huiga sauti ya kitu (Msokile, 1993). Matumizi ya tanakali sauti yanamfanya msomaji

aendelee kusoma riwaya na kupata ujumbe uliokusudiwa na mwandishi. Mwandishi katika kazi yake, ametumia tanakali sauti ka kumtumia mhusika wake akieleza hivi;

> Wale watu wawili waliokuwa wanaonekana vivuli, walisemezana kwa sauti za chinichini "Nadhani huyo mzee amefika". Mwenzake ambaye naye alikiona kivuli cha mtu kikikaribia pamoja na sauti ya kacha-kacha ya majani iliitikia "kweli ni yeye." Walisimama kwa pamoja kunisubiri akaribie (2008:28).

Katika dondoo hili, tunaona jinsi mwandishi anavyoweza kuibua dhamira alizokusudia ziifikie hadhira yake kwa kutumia tanakali sauti kulingana na mazingira ambamo tanakali sauti hizo zimetumika (Omary, 2011). Hapa katika dondoo hili, tunaona kuwa, tanakali sauti zimesikika au kutumika kwenye mazingira ya kuwepo kwa majani au nyasi, mazingira ambayo, mwandishi asingeweza kutumia tanakali sauti nyingine tofauti na hiyo ya kachakacha ili kuhitimisha azma yake ya dhamira aliyokusudia. Hapa na pale, tunamwona mwandishi akiendelea kutumia tanakali sauti kwa kutumia usanii wake kwa lengo la kuendeleza dhamira alizokusudia.

Matumizi ya tanakali sauti hayakuishia kwenye riwaya ya *Vipuli vya Figo* tu, bali pia kwenye *Siri za Maisha*; mwandishi kwa kutumia usanii wake anasema:

> Mwanga ule wa Melkizedeki ulijaa chumba Kizima. Hakika ilikuwa nuru ya kuvulia. Pama alimtazama Brenda pale kitandani. Alikuwa fofofo. Nuru ya rangi za Melkizedeki zilimtambaa kutoka kifuani hadi kichwani akaonekana amependeza sana (2010:08).

Kwa kawaida, tanakali sauti hujitokeza katika mazingira ya kuwepo kwa kitu au wakati tendo fulani linapotendeka (Msokile, 1992).Melkizedeki alipoingia chumbani kwa Pama, Brenda hakumwona kutokana na usingizi mzito aliokuwa nao ambapo

mwandishi ameuelezea kwa kutumia tanakali sauti kwa lengo la kuwashawishi wasomaji ili waweze kugundua dhamira aliyokusudia mwandishi.

### 4.3.5 Matumizi ya Lugha yaKitaharuki katika Riwaya Teule

Taharuki ni ile hali ya matarajio ambapo tuna hamu ya kutaka kujua kitakachotokea baadaye. Kimsingi, hii ni hali ya kusisimua inayompata na kumshika msomaji kiasi cha kuwa na hamu kubwa ya kujua hatima au mambo ya baadaye (Wamitila, 2002).Ujengaji wa Taharuki hutofautiana kutoka mtambaji mmoja hadi mwingine, hata kama kisa kinachoelezwa ni kile kile kimoja. Mtambaji mwenye ujuzi, uzoefu na kipawa zaidi atafaulu kuishikilia hadhira yake katika uzi wa taharuki zaidi ya yule ambaye ndio kwanza anaingia ulimwengu wa utambaji. Ufundi wa kuishikilia hadhira katika taharuki unaweza kuletwa si kwa yale yanayoelezwa tu bali pia jinsi yanavyotolewa na mtambaji. Mabadiliko ya sura ya mtambaji, kwa mfano huweza kuifanya hadhira ijue kuwa jambo litakaloelezwa baada ya muda mfupi ni la kutisha, kwa hiyo wawe na taharuki na ari ya kulisubiri.

Mbinu nyingine itumiwayo pia katika fasihi andishi ili kuumba hali taharuki ni ile ya kuchelewesha matukio fulani au majibu ya maswali flani ambayo msimuliaji huyafanya yawazukie wasikilizaji au watazamaji wake.Haya hucheleweshwa hadi baadaye sana wakati ambapo hadhira huwa imekwishaning'inia katika kamba ya taharuki kwa muda mrefu (Senkoro, 2006:29).

Maelezo ya wataalamu hawa yana umuhimu mkubwa tunapozungumzia suala la taharuki katika kazi za fasihi kwa kuzingatia kwamba, msomaji atakapokutana na hali ya taharuki katika hadithi anapatwa na mvuto fulani wa kumshawishi aendelee

kusoma kazi hiyo hadi mwisho. Wasanii waliobobea kwenye fani hii mara nyingi hupendelea kuichora taharuki mwishoni mwa kazi zao ili kumfanya msomaji aweze kutafakari kile alichokisoma ambapo kinaweza kumpatia ujumbe aliyokusudia mwandishi uifikie hadhira yake. Haya yamejitokeza katika riwaya ya *Vipuli vya Figo* pale mwandishi aliposema;

> Magamba hakwenda mara ile ile kule chumba cha kuhifadhia maiti. Badala yake alikaa kitini na mara, kwa namna isiyo ya kawaida, alisikia woga. Woga gani huu? Ulikuwa unatoka wapi? Huyu maiti aliyeletwa na hawa askari ni nani? Kwanini Dkt. Matoga kasema vile? Nywele zilimsimama, naye vilevile Alisimama. Nitakwenda nimwone huyo maiti. Ni nani? Mzee Magamba alitembea pale alipokuwa kwa mwendo Wa kusita. Aliingia kwenye chumba cha maiti. Maiti wengi, Wa kila aina, wa kila umri. Lakini yeye hakuwa na haja na hao Wote. Yeye alikuwa na haja ya maiti mmoja tu. Alisogea na Macho yakatulia juu ya shuka lile jeupe lenye mabakamabaka ya damu. "Kama ni ajali basi itakuwa faida kwangu. Nitamuuzia Sahibu yangu Dkt. Matoga figo na moyo. Na Mungu ampe maisha Marefu Dkt. Matoga. Tukiendelea na biashara yetu hii, Inshallah, Hata nyumba ya pili nitajenga." Mzee Magamba aliwaza yote Haya, akajaribu kunyoosha mkono ukakataa. Ajabu! Mkono Ulikuwa mzito, kwanini? Nje, Magamba alisikia bundi akilia Juu ya paa la mochwari. Lakini hilo halikuwa jambo la ajabu. Mara kwa mara bundi hulialia sana hapa mochwari, na hata mazingira, yote ya Lumumba yamejaa bundi. Hapana, kulia kwa bundi yule kulikuwa si jambo geni. Jambo geni la kushangaza ni kuwa mlio wa bundi Yule haukuwa mlio wa kawaida. Ulikuwa ni mchanganyiko wa mlio wa paka, wa mtoto mchanga na wa bundi mwenyewe. Zilipita sekunde kadhaa hali kasimama tu akisikiliza, kisha kimya. Na kimya kile kilitisha zaidi kuliko mlio ule wa paka__ mtoto__bundi. Maganga alitoa pumzi, akanyoosha mkono na kuifunua shuka. Aafanaleki! Astkafirurahi! Dkt Matoga! … Mzee Magamba alifunika maiti Yule shuka na kutoka nje ili apate upepo; lakini ghafla, hata kabla hajafika nje alipiga mbwewe iliyochanganyikana na kikohozi, kitu fulani kikatumbuka ndani kifuani mwake, na mara mdomo wake, kama bomba la uchafu ulimimina matapishi mbele yake. (2008:260-261)

Katika dondoo hili,mwandishi ameiweka taharuki katika sura ya mwisho kabisa kwa sababu maalumu zinazoweza kumfanya msomaji wa kazi hii aisome hadithi yote ili aone kitu gani kitakachotokea.Emmanuel Mbogo ameichora taharuki kw usanii wa hali ya juu utakaoibua maswali mengi kwa wasomaji wa riwaya hii na kuwafanya waelewe kile alichokusudia mwandishi.

Wasanii wa kazi za fasihi wanapenda kutumia mbinu ya taharuki ili kuwavuta wasomaji waendelee kuzisoma kazi zao. Wamitila (2002) anasema kuwa, taharuki inaleta hamu ya kujua yajayo na kutia hamasa ya kupenda kusoma zaidi.

Taharuki katika *Siri za Maisha* imetumika pale mwandishi aliposema:

> Brenda alichukua muda kuupata ukurasa alipokuwa ameipachika. Alipoiona alitabasamu, “Aa ni hii” Halafu akagutuka “Aa!” “Vipi!” Wageni wote walimuuliza kwa mpigo. Lakini Brenda hakujibu. Alionyesha mstuko na bumbuwazi la kitendawili cha barua ya mumewe. Wageni wote wawili walisimama wakamsogelea. “Barua ndiyo hii?” Waliuliza kwa pamoja. “Ndiyo.” Brenda aliitikia” lakini vipi? Mbona imegeuka majivu? Na wala haisomeki, aliongeza mama Leah na katika kimya kile cha tafakari, upepo ulitoka ulikotoka, ukayapeperusha majivu yale chini sakafuni (2010:29).

Kwa kawaida, mbinu ya taharuki inamfanya msomaji aendelee kuisoma kazi ya fasihi mpaka mwisho ili aone kitakachotokea. Kitendo cha barua ya Pama kugeuka majivu, kisha majivu hayo nayo yakapeperushwa na upepo, kiliwafanya jirani zake Brenda kujiuliza maswali na kushindwa kuelewa kitakachotokea. Msomaji yeyote wa kazi za fasihi anapenda aone mwisho wa kazi anayoisoma na kama kazi hiyo haijafikia mwisho, msomaji ataendela kuisoma hadi afike mwisho. Kwa maana hiyo, hii ni mbinu ya usanii wa hali ya juu anayoitumia Emmanuel Mbogo ili wasomaji waendelee kuzisoma kazi zake wapate dhamira alizokusudia.

### 4.4 Dhamira katika riwaya ya *Vipuli vya Figo*na *Siri za Maisha*

Katika sehemu hii, tumefanya uchambuzi wa dhamira zinazojitokeza katika riwaya ya Emmanuel Mbogo kwa lengo la kuona jinsi dhamira hizo zinavyokubaliana na hali halisi ya maisha ya jamii katika mazingira yao ya kila siku. Kwa kawaida, dhamira zinazojitokeza katika kazi ya fasihi ni zile zinazoigusa jamii katika Nyanja zake za kiuchumi, kisiasa, na kiutamaduni ambazo mwandishi ameziibua kwa kutumia lugha ya kisanii na kuweza kufikisha ujumbe kwa jamii husika. Senkoro (1976) katika maelezo anasema kwamba, msanii wa kazi za fasihi hana budi kuwa mwangalifu katika kuchagua dhamira ambazo zimefundisha na kujenga msimamo wa kimaendeleo katika kuikwamua jamii kutoka katika minyororo ya utumwa wa ukandamizwaji.

Anaendelea kusema kwamba, itabidi msanii huyo afanye utafiti wa matakwa na mategemeo ya jamii yake. Dhamira hizo lazima zielezwe kiufundi ili kufanya watu wapende kusoma kazi za sanaa hizo; kama kazi ya sanaa itakuwa na fani duni lakini maudhui yake ni mazuri,basi hata maudhui yaliyokusudiwa hayatatoa ujumbe unaokusudiwa inavyopasa. Au ikitokea maudhui ni duni na fani ni bora, pia jamii itapata hasara ya kufikiriwa na maudhui yasiyo na maana katika jamii hiyo kwa kupitia fani iliyo bora. Kutokana na maelezo ya wataalamu hawa ni kwamba, Emmanuel Mbogo ni miongoni mwa watumizi wa kazi za fasihi hususani riwaya ambayo amefanya utafiti juu ya matakwa ya jamii yake na kuwasilisha dhamira zinazihusu maisha ya jamii yake katika mazingira ya kila siku.

### 4.4.1 Biashara Haramu

Biashara haramu ni ile ambayo inafanywa na mtu au kikundi cha watu bila kufuata taratibu na sheria zilizowekwa katika jamii. Wakati mwingine biashara haramu ni aina ya biashara ambayo imekatazwa kisheria kufanywa lakini baadhi ya watu wanajihusisha katika kuifanya biashara hiyo. Mwandishi Emmanuel Mbogo anatuonesha kuwa, Dkt. Matoga baada ya kufukuzwa kazi, alijiingiza kwenye biashara haramu ya kuuza figo na mioyo ya mwili wa binadamu akishirikiana na M.C.Profesa Williams daktari maarufu huko ughaibuni. Kabla hajaanza biashara hiyo, alifanya marekebisho ya zahanati yake kwa kuongeza baadhi ya vyumba na kuhakikisha anavyo vifaa muhimu kwa kazi hiyo pamoja na wafanyakazi atakaoshirikiana nao katika kazi hiyo.

Katika biashara hiyo, zilitakiwa figo za binadamu pamoja na mioyo kwa ajili ya kusafirishwa kwenda nchi za nje. Dkt. Matoga aliandaa mazingira ya kupata figo hizo kutoka sehemu mbalimbali ambazo watu wasingetilia mashaka jambo lolote. Baadhi ya sehemu alizokusudia kupata bidhaa hizo ni Mochwari, magereza kwa wafungwa pamoja na maeneo yaliyokuwa yanakaliwa na watu maskini waliokuwa hawana nyumba za kulala zaidi ya vibanda vya muda walivyojenga kwa makaratasi. Biashara ya aina hii haina tofauti na ufisadi wa kuiba rasilimali za umma kwa masilahi binafsi unaofanywa na viongozi (Mwaifuge, 2006).

Biashara haramu iliyokuwa inafanywa na Dkt. Matoga inajidhihirisha katika dondoo lililopo hapa chini kama ifuatavyo:

> Nyau aliteremka na kufunga geti la machinjoni na maraAkaingiza gari. Waliipakua ile shehena ya vipuli vya familiaMoja ambayo bado ilikuwa imelala na kuimwaga ndani

> ya Friji moja. “Sasa?” Aliuliza Shipe. “Sasa nini?” Lete msumeno”,akaulenga meno yake juu ya kile kichwa kwa zamu; akabonyezaKraa raa raa! Kraa! Kraa! Alichungulia kidogo mle ndani akaona Damu na ubongo vinafoka; akafunga lango la friji. “Tayari.” Alisema. “Twende zetu (2008:164).

Dondoo hili linaonyesha hali halisi ya kupatikana kwa bidhaa zilizofanikisha biashara haramu ambayo Dkt. Matoga aliendesha kwa kutumia watu mbalimbali ambao wangeweza kupata figo za binadamu pamoja na mioyo kwa njia ya mauaji ya kikatili kufanikisha biashara yake. Jambo la kushangaza na kusikitisha ni lile linaloonyesha mazingira ya kupatikana kwa vipuli hivyo ambapo ni ukiukahi wa haki za binadamu, kwamba mtu asiyekuwa na kipato hana haki ya kuishi. Watu walioonekana hawana mahali pa kulala walikumbwa na biashara hii kama mwandishi alivyosema:

> Nenda mbali kidogo,alisema Nyau. “Kuna wengine huwa wanalala pale kwenye vibanda vya makaratasi.” Landrover iliongeza mwendo na mara mbele yake, vilionekana vibandavya makaratasi na vipande vya mabati. Huu ulikuwa uwanja katikati ya supamaketi na posta, hivyo maskini wengi walijengavibanda vya makaratasi usiku ili wajipatie usingizi humo. Keshoyake walivibomoa na kuyaweka vizuri maboksi na makaratasi yao mahali ambapo yasingenyeshewa na mvua. Halmashauriya jiji imejaribu mara kwa mara kuwafukuza maskini hao wasijenge wala kulala hapo, lakini baada ya muda vibanda hivyoviliibuka tena vingi kama uyoga. Landrover ilisimama na kabla wawindaji wale watatu hawajatoka, Nyau alisema, “Sikilizeni.Kwanza tutapita kila kibanda tunapulizia nusukaputi ya kutosha Kuhakikisha kuwa wote wanazimia. Kisha Kipanga utasogeza gari hadi karibu kabisa ili iwe rahisi kuwapakia. Hapa tutapata vipuli vingi sana”. Kweli, alikubali Shipe. “Na sijui kama gari litatosha kuwapakia wote?” (2008:164-165).

Katika dondoo hili,tunaona mazingira yaliyowekwa kwa ajili ya kupata vipuli. Haya yalikuwa ni mazingira yaliyokiuka haki za binadamu na kuukana utu wa binadamu pia. Sengo (1973) katika kufafanua dhanna ya “Mtu ni Utu” anasema kwamba,mtu ndiyo msingi,ndiyo nguzo na ndicho kitu kinachomjenga mtu kuwa kama alivyo; na

kwa hivyo hutofautiana na viumbe wengine. Maelezo ya mtaalamu huyu yana umuhimu mkubwa wa kuweza kutafakari unyama waliokuwa nao hawa wafanyakazi wa Dkt. Matoga, unyama wa kutokuwaona watu waliolala kwenye vibanda vya makaratasi ni binadamu kama wao walivyo. Dondoo hili linatufanya tujiulize maswali kwamba, Dkt. Matoga mbali na kuwa daktari aliyemiliki zahanati yake mwenyewe, bado hakuona biashara nyingine ya kufanya isipokuwa hiyo ya kutoa roho za watu iliapate figo na mioyo?

Watu wanaamini kwamba, daktari ndiye mtu pekee wa kuweza kutatua matatizo ya wagonjwa na kuleta uponyaji lakini Dkt. Matoga amekuwa kinyume cha matarajio haya na badala yake analeta maangamizi na kusahau kabisa utu. Biashara haramu kwenye jamii yetu ya Kitanzania ipo na inapigwa vita na vyombo vya dola pamoja na jamii kwa ujumla kwa kuwa inakikuka haki za msingi za binadamu. Ni biashara inayofanywa na baadhi ya kikundi cha watu wachache ambao jamii ikishirikiana kwa pamoja na kuelekeza nguvu zake zote katika kuipiga vita, hakika haitaweza kuendelea na matokeo yake utu wa binadamu utaonekana kwa jamii nzima.

### 4.4.2 Umuhimu wa Elimu katika Jamii

Dhamira ya Elimu imechukua nafasi katika riwaya ya *Vipuli vua Figo* kwa kuzingatia kuwa, Emmanuel Mbogo pamoja na kuwa ni msanii wa kazi za fasihi lakini pia ni mdau katika Nyanja ya elimu kwani kwa kupitia karamu yake amefanikiwa kuelimisha jamii. Kwa kutumia usanii wake wa riwaya na tamthiliya. Suala la elimulimethaminiwa na watu wengi hususani wasanii wa kazi za fasihi, miongoni mwao akiwa Shaaban Robert (1991) aliyetambua umuhimu wake na kuona

kitu muhimu cha kumpa binti yake siyo fedha wala mali bali ni usia unaohusu **elimu**,kwamba kwa kuitumia **elimu** anaweza kumshauri mtu akapata aliposema;

Elimu ni kitu kizuri, Kuwa nacho Ni fahari,Sababu humshaurimtu la kutumia(1991:11).

Suala la elimu limepewa kipaumbele na Emmanuel Mbogo pale alipomtumia mhusika wake akisema:

> Kibao mwanawe Dkt. Matoga, jana hakulalaNyumbani. Amri ilikuwa imetolewa na viongoziwa Chui Football Club kuwa mkesha wa kuamkiaMechi kati yao na Nigeria Morning Stars, wachezaji Wote ili walazimu kulala kwa mganga. Mpaka sasa, Wazimu huu wa mahaba ya kucheza mpira aliouona Babake kuwa ni upotezai wakati alikuwa bado hajaupatiadawa. Alihofu kuwa mwanawe alpoteza nafasi yake nzuri ya masomo na kuwa mtu maarufu maishani. Kama wazaziwengi, Dkt. Matoga alishikilia msimamo wa: Elimu ni ufunguowa maisha. Lakini kibao mwanawe aliona kuwa elimu ilikuwaufunguo mmoja tu kati ya funguo nyingi zinazoweza kumfunguiamtu milango ya riziki na heri maishani. Na moja ya funguo hizo nimpira (2010:25).

Dondoo hili linatujulisha kuwa Dkt. Matoga hakutaka mwanaye kibao ajihusishe na elimu nyingine yoyote zaidi ya inayotolewa darasani ambayo aliamini kuwa, ndiyo elimu pekee inayoweza kumkomboa mwanaye katika maisha yake ndiyo maana akamwambia **elimu ni ufunguo wa maisha.** Lakini kwa upande wingine, katika dondoo hili, tunaona kuwa siyo **elimu** ya darasani tu inayoweza kumkomboa mtu, hata elimu nyingine inayoweza kupatikana katika mazingira ya kila siku kama Kibao alivyoona mpira ndio unaoweza kumpatia mahitaji yake hata kama hataingia darasani. Binadamu anaweza kujifunza kupitia njia mbalimbali kutegemeana na

mazingira anayoishi; lakini kujifunza huku hakumfungi mtu kuingia darasani ili apate upeo mkubwa zaidi kwa yale anayojifunza katika mazingira yake.

Kibao aliuthamini mpira kuliko yale yanayofundishwa darasani, lakini ukweli ni kwamba, mtu anapopata elimu elimu ya darasani ambayo natolewa na wataalamu wa elimu, elimu hiyo itamsaidia kumwongoza katika kupata elimu nyingine katika mazingira anayoishi, elimu kama ya kucheza mpira, biashara na hata elimu ya mazingira katika kupambanua na mambo yanayoharibu mazingira tunayoishi. Dkt. Matoga angemshauri Kibao aendelee na elimu ya darasani na wakati huo huo angemsaidia katika kukuza kipaji chake cha kucheza mpira kwa kuwa alishaona mpira unaweza kumsaidia katika kumudu maisha yake. Kwa upande mwingine, jamii haina budi ikubali kuwa, kila mtoto ana kipaji chake tofauti na cha mwingine; kwa maana hiyo, wazazi,walezi na jamii kwa ujumla wanatakiwa kuwasaidia watoto katika kukuza vipaji vyao, kwa kuwa, kwa kupitia vipaji hivyo, watoto hao wanaweza kupata maisha mazuri hapo baadaye. Emmanuel Mbogo anaendelea kuisawiri dhamira hii kwa kumtumia mhusika wake akisema;

> Sasa alikaa ju ya kiti kilichotengenezwa kwa mitiakayaegesha macho yake kwa mwanawe KibaoKisha TV kisha Kibao tena. “Shule vipi?” “Naam!Kibao aliinua macho na kumtazama babake. “Nakuuliza shule vipi?” “Inaendelea vizuri baba”,Alijibu Kibao huku akihisi kuwa mhadhara kuhusuFaida za masomo na hasara za kucheza mpira Ulikuwa umekaribia. “Lazima ukazanie masomoYako”, alianza babake, “elimu ni ngao ya Maisha!Elimu ni mali! Elimu ni silaha….Unaelewa?” “Naelewa baba”, akiitikia na kuzima ile TV,Maana alimwona babake akitupa macho katiYa TV nay eye kwamba si adabu kumtegea sikioMoja yeye na jingine kwingine. “Ukipata elimuHakuna mtu anayeweza kukupokonya. Ni maliYako kichwani mwako hadi kufa. Unaweza Kuajiriwa kazi mahali popote. UkinyanyaswaOfisi hii, unaweza kukimbilia kampuni ile.Nitazame mimi leo. Juzi nilikuwa daktariLumumba, jana mwanasiasa waziri, na leoSijali, naweza kufanya kazi mahali

> popoteDuniani. Nikitaka kazi Marekani nitapata.Nikitaka Ufaransa, Uingereza, Japan kokoteKwa nini? Kwasababu elimu ninayo. LakiniSina haja ya kwenda ughaibuni, nitayaendeshamaisha yangu hapa hapa nchini. Nitahakikisha kuwa wewe na dada zako mnapata elimu nzurihadi chuo kikuu. Ile zahanati ya mtoni sasa hivinaifanyia upanuzi, na Mungu akijalia, maisha yatakuwa mazuri. Nitanunua viwanja nijengemajumba, mashamba nilime na wanyama nifuge.Unaona? Mali yote hio itakuktaka wewe na kakakoBruno kuitazama na kuitunza wakati mimi na mamakoTutakapokuwa tumezeeka ama tumeiaga dunia. Unaelewa?"Naelewa baba" aliitikia Kibao kwa adabu akawaza moyoni"Ndiyo maana siku zote nakwambia kuwa usipende sana mpiraHautakufikisha mahali popote. "Unaelewa?" Kila mara Dkt MatagaAmefikiri, na kwa makosa makubwa kuwa watoto tu. Hivyo Hahitaji kujadiliana nao maswala mbalimbali kuhusu maisha yao(2008:86-87).

Maelezo ya dondoo hiliyanaonyesha kuwa, Dkt. Matoga amedhamiria kuwapa elimu watoto watoto wake ili hapo baadaye waweze kuitumia elimu hiyokutunza mali yake na iwasaidie katika maisha yao ya kila siku. Jambo ambalo Dkt. Matoga hakulitaka ni majadiliano na watoto wake kuhusu elimu anayoitaka, yaani elimu ya darasani na mambo mengine ya kujifunza kutoka katika mazingira wanayoishi. Kwa upande mwingine, watoto wana nafasi yao ya kujieleza na kupata ushauri kutoka kwa wazazi mara inapobidi, lakini kwa upande wa Dkt. Matoga haikuwa inamfanya mtoto kuwa na hofu nap engine kutoa mawazo yake ambayo wakati mwingine mawazo hayo yanagusa kile mtoto anachopenda ambapo akisikilizwa ataweza kujifunza mambo mengi na kuibua kipaji chake.

### 4.4.3 Malezi katika Jamii

Suala la Malezi hufanywa na watu mbalimbali walioko katika jamii husika. Mtoto anapozaliwa, hulelewa na family akiwepo baba na mama, hadi mtoto anapofikia umri wa kwenda shule, walezi huongezeka kwa kuwa mtoto atakuwa ameingia kwenye

ngazi nyingine kulelewa kimasomo. Kwa maana hiyo, malezi ya mtoto yanaanzia pale mtoto anapozaliwa; kadri anavyokua mtoto huyo, ndivyo anavyofundishwa na kujifunza mambo mbalimbali kutegemea na malezi au wazazi watakavyofundisha na kumwelekeza. Wataalamu wa lugha wana methali isemayo, mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.

Methali hii haiwezi kupingwa na mtu au mlezi yoyote kwa kuwa anajua wazi kwamba, mtoto anafanya yale aliyoelekezwa hadi atakapokuwa mtu mzima. Wapo wazazi ama walezi waliowazoesha watoto wao kuangalia luninga kilasiku bila kujali watoto hao wanatakiwa wawe na muda wakujisomea, muda wa kusaidia kazi za nyumbani na muda wa kulala pia. Kwa kuwa watoto hao wamelelewa hivyo tangu wakiwa wadogo, ni vigumu kubadili tabia hiyo na kujipangia ratiba ya kuangalia luninga, badala yake wataendelea na tabia hiyo hadi wanapokuwa watu wazima; na katika hali hiyo ya utu uzima inakuwa ni vigumu mtu huyo kubadili tabia hiyo. Emmanuel Mbogo amesawiri vilivyo dhamira hii na kusema:

> "Nasikia njaa!" Angel alicheka kidogo, "Twende,Utakula nyumbano". Alimkagua mdogo wake usoni. Nguo za shule zimechafuka kwa wino, vumbi na rangiYa matunda ya zambarau. "Baba amekuja kunichukua?Mimi sipandi mabasi dada". Alinung'unika Sophia. Mtotoumleavyo ndivyo akuavyo. Mtoto Sophia hakujua kuwaule utajiri wa zamani wa magari haukuwa wa babake balikwa dhamana. Serikali ilikuwa imemdhamini Dkt. Matogacheo, magari na marupurupu mengine yamekoma. Lakini mikasa na sababu hizi hata kama Sophia angelielezwa, asingezielewa. Na siku zote heshi kumwuuliza mama na babake:"Baba kwanini tumehama kwenye nyumba yetu nzuri?"Baba kwanini dereva wetu haji tena kunipeleka shule?"Baba hiki, baba kile.Mama vipi! Mama imekuwaje?Ilimradi maswali yasiyo na majibu yalimporomoka kilataabu ilipozidia(2008:41).

Dondoo hili linatupa picha na kutuonyesha malezi waliyolelewa watoto wa Dkt. Matoga hasa mtoto wake wa mwisho Sophia, kwamba aliwalea kifahari akidhani kwamba ataendelea na wadhifa alionao hadi mwisho bila kujua kuna kupanda na kushuka. Watoto wanatakiwa walelewe kwa hali ambayo itawafanya waone kwamba maisha yanabadilika na wakati mwingine mtu anaweza kuwa katika nafasi ya juu bila kutegemea mtu huyo akajikuta amerudi kwenye nafasi ya chini.

### 4.4.4 Siasa na Uchumi katika Jamii

Dkt.Matoga tangu ateuliwe kuwa waziri wa Afya, alishajiunga na Siasa na kuwa mmojawapo wa wanasiasa, siyo kwa lengo la kuwatumikia wananchi wake, bali kwa lengo la kujinufaisha yeye mwenyewe kwa kuwa alishafungua zahanati yake na kuifanyia marekebisho kwa ajili ya kuhudhuria wagonjwa kwa lengo la kumpatia kipato baada ya kuachishwa wadhifa wa U-waziri. Vuguvugu la Siasa lilipamba moto kwa kipindi hicho Dkt. Matoga alikuwa anasoma sana magazeti na kupata habari ambazo kwa namna moja au nyingine aliamini kuwa zingine zingemletea manufaa katika zahanati yake, kwani alijihusisha na biashara ya kuuza Vipuli vya Figo na mioyo ya binadamu na kuvisafirisha kwenda nchi za ughaibuni.

Kwa ujumla, Dkt. Matoga alipendelea mfumo wa vyama vingi ambavyo kwa kawaida vilipingana na chama tawala kilichosimamia Siasa ya ujamaa.Kwa upande wa Dkt. Matoga, aliamini kuwa, kuwepo kwa mageuzi ya Siasa na Uchumi, ambapo mageuzi hayo yangekiondoa chama tawala madarakani, kisha kikatawala mojawapo ya chama cha upinzani, ni wazi kwamba, biashara yake ya Vipuli vya Figo na mioyo ya binadamu ingefanikiwa kwa asilimia kubwa na katika imani yake aliamini kuwa

kuwepo kwa mfumo wa vyama vingi biashara yake ingepata ulinzi. Hayo yamethibitishwa na mwandishi pale alipomtumia mhusika wake akisema:

> Wimbi la demokrasia lilikuwa limepamba moto dunia nzima. La! Sijui hapa kwetu kama huu mtindo wa vyama vingi utatufaa? Aliwaza;kuna ukabila, kuna umaskini, kuna wivu, kuna..., alisita kidogo. Lakini kwa upande mwingine, hili linaweza kuwa jambo zuri.Njia nzuri ya kuhakikisha kuwa utajiri na uhuruwa mtu unalindwa ni kupitia demokrasia yavyama vingi. Ndiyo, dawa ni kujiunga na chamakimoja chenye nguvu na Mungu bariki kamamkishinda, naweza nikajikuta tena niko Bungeniau hata Waziri. Na Siasa ni nini kama siyo pesa?Mipango yangu hii ikienda sawa, haya yote yatanyooka (2008:107 – 108).

Dondoo hili linaonyesha jinsi Dkt. Matoga alivyokuwa na uchu wa fedha kwa kujiingiza kwenye masuala ya Siasa kwa lengo la kufanikisha biashara zake. Wapo watu wanaojiingiza kwenye masuala ya Siasa kama kinga ya shughuli zao ambazo zinakiuka utaratibu uliokuwepo kwa jamii. Watu kama hao wanaliona suala la Siasa ni kama mwamvuli wa kujikinga maovu yao yasigundulike. Akitoa uthibitisho wa kauli hii, mwandishi anasema:

> Katuturu hakujua kuwa mmoja wa wafuasi wake Dkt.Matoga hakuwa amejiunga na True Demokratic Tigers ili hatimaye apande daraja, awe kiongozi mwana siasa katika serikali moja. Ni kwa ajili hii tu ambapo Dkt. Matoga angehakikisha usalama wa utajiri wake; yaani majumba yake, mashamba yake, na hususani madola yake aliyo yakimbiza huko Ulaya na Marekani. Madola yaliyotokana na uhai wa Mioyo na Figo za maskini, Vipofu, Malaya, vichaa, wafungwa waliohukumiwa kunyongwa wenye kupatwa na ajali, vilema…waliozagaa na kutapakaa katika vichochoro, mitaa na mageto ya jiji la Datuta (2008:241).

### 4.4.5 Nafasi ya Mwanamke katika Jamii

Dhamira ya mwanamke na nafasi aliyo nayo katika jamii imemshughulisha sana Emmanuel Mbogo, siyo katika riwaya ya *Vipuli vya Figo* tu bali hata katika kazi zake nyingine za sanaa kama vile tamthiliya kwa kiasi kikubwa hakuweza kukwepa

jukumu hilo. Katika riwaya ya Vipuli vya Figo, mwanamke kwa upande mmoja amesawiriwa kama mtu shupavu anayesimamia vizuri nafasi yake na kujali jukumu lake la kulea familia na kutoa ushauri kila inapobidi kufanya hivyo. Mhusika Ma Angela anawakilisha wanawake waliosoma na mwenye kutoa elimu kwa jamii nyingine hasa wanafunzi wanaochukua nafasi kubwa katika jamii. Dkt. Matoga alipofukuzwa kazi ya Uwaziri na kupata misukosuko ya kisiasa iliyomfanywa kuwekwa ndani, Ma Angela alisimama kidete na kukabiliana na hali hiyo kwa kumshauri mumewe waanze kufungasha mizigo yao kabla askari hawajawatoa kwenye vyumba kwa nguvu. Emmanuel Mbogo, anaeleza kwamba, baada ya Dkt. Matoga kufukuzwa kazi na kunyang'anywa gari pamoja na nyumba ya kifahari walimokuwa wanaishi, mkewe alisimama kwenye nafasi yake kama mshauri wa mumewe na kusema:

> Nimewaambia watoto waanze kufunga mizigoChalo nimemtuma aende kunnua maboksihapo supamaketi. "Tunakwenda wapi?" Aliuliza Ma Angela sauti imepungua hamaki.
>
> "Sijui. Nadhani tunaweza kwenda kukaa hotelikwa muda-pesa ninazo kabla hatujapata nyumba ya kupanga mahali pengine." "Mm! Wewe una mawazo gani?" "Bwana, hotelini na watoto wote itakuwa ghali sana, heri kwenda kwa mjomba. Kama kuna kubanana, tutabanana hivyohivyo kuliko hotelini (2010:16).

Katika hili, tunamwona Ma Agela akisimamia zoezi zima la kufungasha mizigo kwa ajili ya kuhamia kwa mjomba wake ambaye alishaona kwamba pasingekuwa na pingamizi lolote la kuhamia huko. Hali hii ya kujiamini kwa Ma Angela na kuwa na uhakika wa kile anachokifanya ilileta faraja kwa familia yake na kuondoa wasiwasi waliokuwa nao watoto wake kwa kudhani wasingeweza kupata mahali pa kwenda kukaa kwa wakati ule. Emmanuel Mbogo anaendelea kusawiri nafasi ya mwanamke

kwa kuonyesha wajibu wake kwa familia na kama mzazi wakati alipomfuata mumewe aliyekuwa amezama kwa Agnita na kuendeleza starehe zake bila kujali mtoto wake aliyekuwa mgonjwa. Katika kutekeleza jukumu lake, na kuonyesha ujasiri aliokuwa nao, Ma Angela alimfuata mumewe nyumbani kwa Agnita, bila kujali kama Agnita angemfukuza au la. Emmanuel Mbogo anasema:

Ma Angela alipanda ngazi hadi ghorofa ya tatu

> akasimama mkabala na mlango. Aligonga mara mbili kisha akafunguliwa. Agnita alishtuka kumwona mke mwenza kasimama mlangoni. Aliduwaa kidogo, kisha, bila kujua anafanya nini, aliufungua mlango zaidi na pasipo neno lolote kutoka kwa kila mmoja wao. Ma Angela aliingia na kukaa kwenye kochi, karibu na mlango. Dkt. Matoga kama mtu aliyenaswa na umeme alikauka pale kwenye sofa, mdomo wazi. (2010: 216 – 217)

Dondoo hili linathibitisha ujasiri aliokuwa nao Ma Angela kwa kuwa alikuwa anajua wajibu wake na Dkt. Matoga ni mumewe na siyo wa Agnita. Kitendo cha Ma – Angela kukabiliana uso kwa uso na Agnita bila kufanya fujo wala ugomvi, kilimfanya Dkt. Matoga ashikwe na bumbuwazi na kumweka Agnita kwenye wakati mgumu; kwani alitegemea Ma – Angela angefanya fujo na pengine kusababisha ugomvi. Kwa hali hii inaonyesha kwamba, mtu mstarabu anapotaka kufanya jambo, anavuta subira na kutafakari kama jambo analotaka kufanya litaleta athari yoyote. Kwa vile Ma Angela alikuwa na mtoto mgonjwa aliyelazwa hospitali, jambo la msingi lilikuwa ni kumhudumia mtoto na siyo kupoteza muda kwa kugombana. Haya yote Ma Angela ameweza kuyatekeleza kwa kuwa aliweza kusimama kwenye nafasi yake kama mwanamke.

Usawiri wa nafasi ya mwanamke katika jamii unajitokeza pia katika riwaya ya Siri za Maisha kama asemavyo mwandishi Emmanuel Mbogo:

> Pama hakujibu ila gafla joto la woga na hofu lilimvaa na mara akaanza kupiga kwikwi akilia. Machozi mengi yalimtiririka. Hakika ghafla alifadhaika kwa kumwona mumewe katika hali ile. Alipga magoti mbele ya mumewe pale kitandani akimdadisi na kumuuliza, "Vipi?" umekuwaje? Ee? Una nini? Mumewangu? Unaumwa? (2010: 11).

Hapa katika dondoo hili tunamwona Brenda akishirikiana na mumewe kwa kutaka kujua yaliyomsibu, akiwa na lengo la kumsaidia kutatua tatizo lililompata ingawa Brenda alikuwa hajui tatizo la mumewake. Brenda alipokuwa na mumewe kabla ya kupatwa na masaibu hayo hakuona kama mumewe alikuwa na tatizo lolote. Wala mumewe hakuwa mgonjwa; lakini ghafla alibadilika akaanza kulia kwa kwikwi bila kumueleza mkewe yale yaliyomsibu. Kwa maana hiyo, mwanamke anayejua wajibu wake kama Brenda asingeweza kuivumilia hali hiyo (2010:11).

Mwandishi anaendelea kusawiri dhamira hii kwa kuonyesha ujasiri na ushirikiano wa Brenda na jirani zake baada ya mumewe kutoweka na kwenda asikokujua. Katika hali hii ya kutatanisha, Brenda alivaa ujasiri, akafungua mlango ili kuona kama Pama alikuwa ametoka nje, lakini hakumwona hata baada ya kuamua kumtafuta. Ujasiri wa Brenda umejitokeza pale alipokwenda kumuamsha jirani yake na kumweleza tatito lake. Mwandishi kwa kuthibitisha haya anasema:

> Ghafla alisimama. "Nitakwenda nimwamshe jirani," aliwaza. Jirani yao alikua Mzee Kiama aliyeishi na mkewe Mama Leah nyumba ya pili (2010:21).

Katika dondoo hili, mwandishi anaeleza jinsi Brenda alivyotambua nafasi yake. Alionyesha ujasiri wa kwenda kumweleza jirani yake kuhusu tatizo lililompata bila kujali kuwa ilikuwa ni usiku.

#### 4.5.6 Hali ngumu ya Maisha katika Jamii

Hali ngumu ya maisha inaweza kusababishwa na mambo kadha wa kadha kama vile ukosefu wa kazi za kuajiriwa, mshahara mdogo anaolipwa mfanyakazi, watu kutojishughulisha na kazi za kuajiriwa wenyewe, mtu kushindwa kupangilia kwa usahihi mshahara anaopata na mengineyo mengi. Hali ngumu ya masiha imejitokeza kwa Pama kiasi cha kushindwa kulipa kodi ya nyumba kwa kuwa alishindwa kupangilia mshahara aliokuwa analipwa na mwajiri wake Sunche Kapeto. Mara nyingi, mtu anapokabiliana na ugumu wa maisha na wakati huohuo analojukumu linalotakiwa kutekelezwa kwa kutumia fedha, mtu kama huyo anasongwa na mawazo na kujikuta anashindwa kuyamudu maisha. Hali hii ilipomkuta Pama alishindwa kuhisi hata utamu wa muwa aliokuwa anautafuna kwa kuwa akili yake ilidhibitiwa na mawazo mengi aliyokuwa nayo. Mwandishi ameisawiri vilivyo dhamira hii kwa kumtumia mhusika wake na kusema;

> Pama aligeuka nyuma akaona ndoo ya Plastiki, akaigeuza akakaa na kuanza kula miwa yake. Lakini kwa hakika akili zake hazikusajili utamu wa muwa mdomoni mwake; kwani uwezo wa kionjo cha ulimi wake kudhibitishwa na tafakari zilizotamalaki akilini (2010:4).

Katika dondoo hili tumeelezwa kwamba, hali ngumu ya maisha inaweza kumfanya mtu asiweze kufikiri vizuri kutokana na Ubongo wake wa fahamu kusongwa na mambo mengi kuhusu hali ngumu anayokabiliana nayo. Ingawa Pama alikuwa mfanyakazi wa kuajiriwa, mshahara aliokuwa anapata haukuweza kutosheleza katika kutatua matatizo ya kifamilia; badala yake aliishia kuwaza namna ambavyo angeweza kuyamudu maisha. Wakati mwingine, hali ngumu ya maisha inaweza kumfanya mtu akakosa usingizi kama ilivyokuwa kwa Pama wakati akiwa amelala. Mwandishi anaendelea kusawiri dhamira hii na kusema:

> Ilikuwa yapata saa nane za usiku. Nje kulikuwa kimya kabisa. Pama usingizi ulikuwa umepaa; alilala chali akiwaza. Mkewe Brenda alilala ubavuni pake akiupiga usingizi mzito. Walisikika mbu wakiimba na kuruka huko na huko gizani lakini hawakuweza kuwafikia hawa wawili; waliokuwa ndani ya kiota cha chandarua. Pama aliwaza kuhusu Pesa, hakuwa ameridhika na mshahara aliopewa na tajiri wake Sunche Kapeto (2010:07).

Katika dondoo hili, mwandishi anatueleza kuhusu ugumu wa maisha ambao Pama alipambana nao; lakini hajatueleza hatua yoyote aliyochukua Pama katika kujikwamua na maisha. Tena anaongezea kwa kusema kwamba, Pama hakuridhika na mshahara aliokuwa anapewa, jambo ambalo lilimletea kusongwa na mawazo kiasi cha kukosa usingizi. Hali kama hii ya ugumu wa maisha siyo ngeni kwa jamii yetu ya Tanzania kwa kuwa wapo watu wanaopata mishahara midogo isiyoridhisha lakini hawachukui hatua yoyote ya kukabiliana na hali hii, badala yake wanabaki wakinung'unika. Nafikiri, jambo la msingi ni kutafuta namna ya kukabiliana na hali hii kwa kufanya kazi nyingine za kujiajiri ili kuongeza kipato badala ya kuishia kulalamika kama Pama.

## 4.6 Hitimisho

Katika sura hii tumechambua, kuwasilisha na kujadili data za utafiti ambazo zimepelekea kukamilika kwa malengo ya utafiti. Madhumuni mahususi ya utafiti huu yamekamilika pamoja na maswali ya utafiti kujibiwa kama inavyotakiwa. Uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti ulifanywa kwa kuzingatia madhumuni mahususi ya utafiti ambapo katika lengo mahususi la kwanza tumechambua matumizi ya lugha ya kitamathali ya tashibiha, tashihisi, tafsida, sitiari, kejeli na dhihaka. Matumizi ya lugha yasiyo ya kitamathali yaliyojitokeza katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha* ni misemo, nahau, takriri, tanakali

sauti na matumizi ya lugha ya kitaharuki. Baada ya hapo tumewasilisha dhamira za biashara haramu, umuhimu wa elimu katika jamii, malezi katika jamii, siasa na uchumi katika jamii, nafasi ya mwanamke katika jamii na hali ngumu ya maisha katika jamii. Hii inatoa ithibati kwamba, madhumuni mahususi ya utafiti huu yamekamilika na kwa hiyo lengo kuu la utafiti nalo limekamilika.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Sura hii ndiyo ya mwisho katika utafiti wetu. Kwa kuzingatia hilo, sura hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu. Kwanza, ni sehemu inayohusu muhtasari, pili ni sehemu inayohusu hitimishi la utafiti huu, na mwisho, ni sehemu inayohusu mapendekezo ya utafiti kwa ajili ya utafiti wa baadaye.

## 5.1 Muhtasari

Utafiti huu umekamilika baada ya kutimizwa malengo mahususi matatu ya utafiti ambayo ni: kuchambua matumizi ya lugha ya kitamathali katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*,kuchambua matumizi ya lugha yasiyo ya kitamathali katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*, na kuwasilisha dhamira kutoka katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*. Kukamilika kwa malengo haya mahususi kuliwezesha kujibiwa kwa maswali ya utafiti huu ambayo yalikuwa: Ni vipengele gani vya matumizi ya lugha ya kitamathali vilivyotumika katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*? Ni vipengele gani vya lugha isiyo ya kitamathali vilivyofafanuliwa katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*? Ni dhamira zipi zilizowasilishwa katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*?

### 5.1.1 Matumizi ya Lugha ya Kitamathali katika Riwaya Teule

Utafiti huu umegundua kuwa mwandishi ametumia tamathali za semi katika riwaya za *Vipuli vyaFigo* na *Siri za Maisha*. Tamathali za semi zilizowasilishwa ni pamoja na tashbiha au mshabaha, tashhisi, tafsida, sitiari, kejeli au kinaya na dhihaka.

Tamathali hizi zilitumika katika kuibua dhamira mbalimbali zinazojitokeza kwenye riwaya hizo.

### 5.1.2 Matumizi ya Lugha yasiyo yaKitamathali katika Riwaya Teule

Utafiti huu umebaini pia kuwa, mwandishi ametumia lugha isiyo ya kitamathali sambamba na mbinu za kisanaa ambazo kwazo dhamira mbalimbali ziliweza kuibuliwa. Lugha isiyo ya kitamathali ni pamoja na misemo, nahau, takriri, tanakali sauti na taharuki. Kupitia matumizi haya ya lugha mwandishi ameweza kuwasilisha dhamira mbalimbali kama zilivyowasilishwa katika uchambuzi wa data.

### 5.1.3 Dhamira katika Riwaya Zilizoteuliwa

Katika kuwasilisha dhamira zilizojitokeza kwenye riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*, utafiti huu umebaini kuwa, dhamira zifuatazo zimebainishwa. Dhamira hizo ni Biashara haramu, Elimu katika jamii, Malezi katika jamii, Siasa na Uchumi, Nafasi ya mwanamke na Hali Ngumu ya Maisha. Dhamira hizi zimebeba uhalisia katika maisha ya kila siku ya jamii ya Kitanzania kutokana na kushabihi namna watu wanavyoishi katika jamii.

## 5.2 Hitimisho

Kwa ujumla utafiti huu umefanikiwa kutimiza madhumuni yake mahususi ambayo yalikuwa matatu na kujibu maswali ya utafiti yaliyokuwa matatu. Dhumuni mahususi la kwanza lilikuwa ni kuchambua matumizi ya lugha yakitamathali katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha* Matokeo ya utafiti wa dhumuni mahsusi la kwanza yameonyesha kuwa, riwaya zote mbili kwa pamoja zimetumia tamathali za semi kwa kiasi kikubwa katika kuwezesha kuibua dhamira zilizojitokeza.

Dhumuni mahsusi la pili lilikuwa ni kufafanua matumizi ya lugha yasiyo ya kitamathali katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*. Matokeo ya utafiti huo yameonyesha kuwa, kwa kiasi kikubwa riwaya zote mbili zimetumia lugha isiyo ya kitamathali katika kusaidia kujenga dhamira zilizojitokeza. Matumizi ya lugha isiyokuwa ya kitamathali imesaidiana na matumizi ya lugha ya kitamathali na kuweza kujengwa kwa dhamira mbalimbali katika riwaya mbili zilizoteuliwa. Matokeo zaidi yanapatikana katika sura ya nne ya tasinifu hii.

Dhumuni mahsusi la tatu lilikuwa ni kuwasilisha dhamira kutoka katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha*. Matokeo ya utafiti huo yameonyesha kuwa, riwaya zote mbili zinasawiri dhamira mbalimbali ambazo baadhi yake zinasawiri uhalisia wa jamii ya Kitanzania. Dhamira zilizosawiriwa katika riwaya za *Vipuli vya Figo* na *Siri za Maisha* ni pamoja na: Biashara haramu, Elimu katika jamii, Malezi, Siasa na Uchumi, Nafasi ya mwanamke na Hali ngumu ya maisha.

## 5.3 Mapendekezo

Utafiti kama huu wa kuchunguza matumizi ya lugha ya kitamathali katika riwaya ya Kiswahili unaweza kufanywa kwa kulinganisha na kulinganua riwaya ya Emmanuel Mbogo na kazi nyingine za mtunzi wa riwaya ya Kiswahili.

Utafiti kuhusu matumizi ya lugha kwa ujumla katika riwaya za Emmanuel Mbogo unaweza ukafanywa katika ngazi ya shahada ya Uzamili na Uzamivu. Utafiti wa aina hii unaweza kuhusisha riwaya zaidi ya mbili za mtunzi huyu.

Utafiti zaidi unaweza kufanyika katika kuchunguza riwaya za Emmanuel Mbogo kama riwaya za Kisaikolojia kutokana na riwaya hizo kuonekana kuwa ni za mkondo huo.

## MAREJELEO

Abdallah, A.O. (2014), "Kuchunguza dhamira za Kijamii na Kiutamaduni katika Riwaya za Shafi Adam Shafi: Mfano wa *Kuli* na *Vuta N'kuvute*," Tasinifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Akhmanova, O. (1992), *Learning a Foreign Language: The Cognitive Approach in Essays in English as a Foreign or Second Language*. New York: Sage Publication.

Babbie, E. (1999), *The Basics of Social Research*, Belmont: Wadsworth Publishing Company.

Barthes, R. (1994), *The Semiotic Challenge*, Berkely: University of Califonia Press.

Barwise, J. and Perry, J. (1983), *Situations and Attitudes*, Cambrige: Mass MIT Press.

Blonsky, M. (1991), *On Signs*, Baltimore: The Johns Hopkins University Press.

Chachage, S.C. (2002), *Makuadi wa Soko Huria*, Dar es Salaam: E&D Company.

Cherry, C. (1966), *On Human Communication*: Cambrige: Mass MIT Press.

Chuachua, R. (2011), *Itikadi katika Riwaya za Shaaban Robert*, Dar es Salaam: TATAKI.

Creswell, J.W. (2009), *Research Design: Qualitative, Quantitative, and Mixed Methods Approaches*, Los Angeles: SAGE Publications.

Eco, U. (1976), *A Theory of Semiotics.* Bloomington: Indiana University Press.

Frenkel, R.J. (2002), *How to Desing and Evaluate Research in Education*, New York:Mac. Graw Hill.

Frutiger, A. (1989), *Signs and Symbols*, New York: Van Nostrand.

Kezilahabi, E. (1971), *Rosa Mistika*, Dar es Salaam: DUP.

Kezilahabi, E. (1976), "Shaaban Robert Mwandishi wa Riwaya," Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Kezilahabi, E. (1983), "Utunzi wa Riwaya na Hadithi Fupi," katika, *Makala za semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili namba 3*, Dar es Salaam: TUKI, Kur. 226-243.

Khatibu, M.S. (1986), Tamathali za Semi za Kiswahili," katika *Mulika* namba 18, Dar es Salaam: Tuki, Kur. 1-15.

Kitereza, A. (1980),*Bwana Muyombekele* na *Bibi Bugonoka*, Juzuu no.2, Dar-es-Salaam: Tanzania Publishing.

Kothari, C. R. (2008), *Reserch Methodogy: Methods and Techiniques*, New Delhi: New Age Internationl Publising Ltd.

Madumullah, J.S. (2009), *Riwaya ya Kiswahili, Historia na Misingi ya Uchambuzi*, Nairobi: Sitima Printers and Stationary.

Mbatiah, M. (1998), "Mienendo Mipya katika Uandishi wa Kezilahabi: *Nagona* na *Mzingile*," Katika *Mulika* namba 24, TUKI, Kur. 1-11.

Mbogo, E. (2008),*Vipuli vya Figo*, Dar es Salaam: East African Educational Publishers.

Mbogo, E. (2010),*Siri za Maisha*, Dar-es-Salaam:E&D Vision Publishing.

Mjema, R. (1990), "*Kusadikika*," katika *Mulika* namba 22, Daer es Salaam: TUKI, Kur. 26-31.

Mlacha, S.A.K. (1987) "The Portrayal of Cultural Conflict in Kiswahili Prose Fiction; A Structual Study of the Novels of Euphrase Kezilahabi" Phd. Thesis, University of London.

Mlacha, S.A.K. (1989), "The Use of Methaphor in Kezilahabi's Novel: *Rosa Mistika*," katika *Kiswahili*, Juzuu namba 56, Dar es Salaam: TUKI, Kur. 25-35.

Mlacha, S.A.K. (1996), "Utamaduni wa Mwafrika katika Riwaya ya *Bwana Myombekere* na *Bibi Bugonoka*," katika, *Mulika* namba 23, Dar es Salaam: TUKI, Kur. 24-35.

Mlacha, S.A.K. na J.S. Madumulla, (1991), *Riwaya ya Kiswahili*, Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mohamed, M. (2006), Mtindo katika Riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote*," katika *Kioo cha Lugha*, Juzuu namba 4, Dar es Salaam: TUKI, Kur. 1-12.

Mohochi, E.S. (2000), "Usimulizi wa Riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini*," katika, *Nordic Journal of African Studies,* 9 (2):49-59.

Mrikaria, S.E. (2010), "Kejeli na Fasihi ya Kiswahili Tanzania," Katika *Swahili Forum*, 17: 104-125.

Mulokozi, M.M. (1990), "Utunzi wa Riwaya ya Historia," katika *Mulika* namba 22, Dar es Salaam: TUKI, Kur. 1-10.

Mulokozi, M.M. (1996), *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*, Dar es Salaam: TUKI.

Msokile, M. (1992), *Kunga za Fasihi na Lugha*. Dar es Salaam: Education Publishers and Distributor, Ltd.

Msokile, M. (1993), *Miongozo ya Lugha na Fasihi: Uchambuzi na Uhakiki wa Riwaya*, Dar es Salaam: DUP.

Mwaifuge, E. S. (2006), "Fasihi ya Kiswahili na Rushwa Tanzania: Thomas A. R. Kamugisha na *Kitu Kidogo Tu*," katika, *Kioo cha Lugha*, Juzuu namba, 4, Dar es Salaam: TUKI, Kur. 39-45.

Nazarova, T. (1996), *Linguistics and Literary Semiotics*, Moscow: Moscow State University Press.

Ndungo, C. (1991), *Misingi na Nadharia ya fasihi ya Kiswahili*.Nairobi:JKF.

Njogu, K. na Rocha, C. (1999). *Ufudishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu.* Nairobi: JKF.

Nkwera, F.V. (1989), *Sarufi na Fasihi: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Omari, S. (2009), "Tanzania Hip Hop As Popular Literature", Unpublished PHD. *Thesis UDSM*.

Omary, M. (2011), "Siasa katika Ushairi wa Kezilahabi," Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Robert, S. (1951), *Kusadikika*, London: Nelson.

Robert, S. (1951), *Adili na Nduguze*, London: Macmillan.

Robert, S. (1958), *Wasifu wa Siti Binti Saad: Mwimbaji wa Unguja*, London: Thomas.

Robert, S. (1967), *Kufikirika*, Nairobi: OUP.

Robert, S. (1968), *Siku ya Watenzi Wote*, London: Nelson.

Robson, C. (2007), *How to do a Reserch Project*: A Guide for Undergraduate Students, Carton Victoria: Blackwell Publishing.

Sebeok, T. A. (1979), *The Sign and its Masters*, Austin: University of Texas Press.

Sengo, T.S.Y.M. (1973a), "Mtu ni Utu (G. Mhina)," katika *Hisi Zetu*, Dar es Salaam: TUKI.

Sengo, T.S.Y.M. (1973b), "Dhima ya Fasihi kwa Maendeleo ya Jamii," katika *Jarida la Kiswahili*, Dar es Salaam: TUKI.

Sengo, T.S.Y.M. (2009), *Sengo na Fasihi za Kinchi*. Dar es Salaam: AKADEMIYA

Senkoro, F.E.M.K. (1976), "Utamaduni katika Riwaya za Kiswahili," katika *Kiswahili*, Juzuu namba 46/2, Dar es Salaam: TUKI, Kur. 74-82.

Senkoro, F.M.E.K. (1982), *Fasihi*. Dar es Salaam: DUP.

Senkoro, F.E.M.K., (2006), "Fasihiya Kiswahili ya Majaribio: Makutano baina ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi", katika, *Kioo cha Lugha*, Juzuu, 1. Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam uk. 61-68.

Shivji, I. (2002), "Makuadi wa Soko Huria (Chachage, S. Chachage), Hotuba ya Uzinduzi wa Kitabu," katika *Mulika* namba 26, 2000-2002, TUKI, Kur. 93-97.

TUKI (2004),*Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Dar es Salaam: TUKI.

TUMI (1992), *Kiswahili Vyuoni*, Dar-es-Salaam: TUMI.

Wamitila, K.W. (2002), *Uhakiki wa Fasihi*: *Misingi na Vipengele Vyake*, Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K.W., (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*, Nairobi: Vide-Muwa.

Waugh, L. R. (1984), "Some Remarks on the Nature of the Linguistic Sign," In *Sign, System and Function*. The Hague: Mouton.

Yin, R. K., (1994), *Case Study Research: Design and Methods,* (2nd eds.) Thousand Oaks Calif: SAGE Publishers.

Young, P.V. (1984), *Scientific Social Surves and Research*, Englewood Chiffs: Prentice Hall. Inc.